Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 74 No. 177 | SAFAR/RABIUL1 1435 AH | JANUARY 2014 | SULH 1393 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini, ingieni nyote katika utii, wala msifuate nyayo za Shetani; bila shaka yeye kwenu ni adui dhahiri.

Na kama mkiteleza baada ya kuwafikieni Ishara zilizo wazi, basi jueni ya kwanba Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima. (2:209-210).

Khalifa Mtukufu ahimiza mabadiliko ya kweli:

Aeleza mbinu za kuleta mabadiliko na kusema, kila kosa ni kosa, liwe kubwa au dogo ni lazima liachwe

Na Mwandishi Wetu

KatikahotubayaIjumaayatarehe 13/12/2013 Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a. alizungumzia juu ya haja na mbinu za kuleta mabadiliko ya kujitakasa nafsi zetu, na alisema:

Katika hotuba zangu mbili za Ijumaa zilizopita nimeendelea kuongelea juu ya somo la kuleta mabadiliko ya kweli, yenye maana na ya kudumu kwa ajili ya kutengeneza nafsi zetu. Katika hotuba yangu ya Ijumaa iliyopita nililieleza somo hili kwa njia ya maswali na majibu kutoka kwenye nasaha za Masihi Aliyeahidiwa a.s. Nilikuwa ninajaribu kufikisha kwa namna ambayo Masihi Aliyeahidiwa a.s. alituongoza kutafakari kwa njia ya maswali iwapo tunafanya mambo haya au la. Ingawaje mabadiliko yetu ya kweli hayatakiwi yabaki kwenye mambo haya machache tu.

Mafundisho ya Islam yanakusanya mambo chungu mzima, kuna orodha isiyo na mwisho ya maelekezo tuliyopewa kutoka ndani ya Qur'an tukufu. Hii ndio sababu Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema katika kitabu chake cha "*Mafundisho Yetu*" na kwa ajili ya manufaa ya kujisuluhisha kwetu: "Ninawaambieni kwa ukweli kabisa yeyote kati yenu ambaye ametenda kosa la hata kutokutekeleza amari ndogo kabisa kutoka kwenye amri 700 zilizomo ndani ya Qur'an tukufu, mtu huyo anajifungia mlango wa uokovu kwa mikono yake mwenyewe." Hili ni jambo linalotakiwa litupe hofu kubwa na tuwe wenye kulitafakari sana. Tunawajibika kushika hadhari ya hali ya juu, kabla hatujishika njia ya kutenda hata jambo dogo kiasi gani.

Niliyasema haya katika hotuba yangu iliyopita pia kwamba lengo la kuja kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. lilikuwa ni kuja kustawisha ufalme wa sheria za Kuran Tukufu juu yetu pamoja na kutuwezesha kuiga mfano wa mwenedo na matendo ya Mtukufu mtume s.a.w. na kwa ajili ya kulifikia lengo hilo Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliendelea kutukumbusha juu ya mambo haya mara kwa mara.

Iwapo tutajichunguza sisi wenyewe kwa uaminifu kabisa, kama nilivyosema awali, tutagundua kwamba zama tunaposikia mambo haya, tunapata mabadiliko fulani lakini mabadiliko hayo hayadumu kwa muda mrefu bali baada ya siku chache watu hurejea kwenye mienendo yao ya nyuma waliyokuwa wamezoea kuendelea nayo. "Hali yetu ni kama ya ule msemo wa Kiingereza kwamba : *Jack* (wakimaanisha mbwa au mnyama wa kufugwa) hubaki kwenye tundu lake muda ambapo litakuwa limefungwa tu, lakini likiwachwa wazi tu mara huruka na kutoka nje"

Basi ndio kama hivyo, muda ambao mada fulani inaendelea kuongelewa watu wengi hubaki wameathirika kwayo lakini mara tu athari ya nasaha hizo ipowapo kwa mazungumzo hayo kusitishwa, basi nao hali zao huwasukuma kuruka nje na kurudi kwenye tabia zao za nyuma na matendo mabaya huonekana yakirudiwa tena.
Marafiki wengi wenye nyoyo zilizohalisika huniandikia kwamba baada ya kusikiliza hotuba zako tunajaribu kujirekebisha na tunaomba na tunakuomba na wewe pia utuombee ya kwamba yule 'jack' ambaye ni sababu ya kuturudisha kwenye maovu asiturejee tena baada ya kufungiwa kwenye tundu kutokana na mawaidha yako.

Kwa vyovyote viwavyo inatulazimu tufikirie sana kwa nini huyu 'jack' anajaribu kila mara kutoka nje ya kasha (tundu). Kuwezekana kwa matengenezo au marekebisho ya kitu chochote na kupatikana athari kwa njia inayotumika hufikiwa tu pale inapoeleweka sababu inayokwamisha matengenezo hayo ili kwamba njia ifaayo ipitwe kumaliza au kuondoa sababu zinazopelekea mapungufu hayo. Iwapo mzizi

Endelea uk. 2

Somo Kutoka Pretoria

Na Mahmood Hamsin Mubiru
Nilipoambiwa niandike juu ya Madiba Mandela nilishika tama! Nilijiuliza mara mbili niandike nini ambacho hakijaandikwa na vyombo vingi vya habari? Gazeti letu la *Mapenzi ya Mungu* linatoka kila mwisho wa mwezi na hivyo kwa fikra zangu niliona hakuna jipya la kusisimua ambalo ningeweza kusema juu ya mwana huyu wa Afrika ambaye amelileta sifa bara hili kwa kugeuza kwa matendo falsafa nyingi za magharibi ambazo zinaelezwa kwa maneno mazuri ya kumtoa nyoka pangoni lakini yenye uhaba wa thamani ya kutekelezwa na hivyo kukumbwa na upepo mbaya unaovuma ukisikitika kwa kusema "Kusema msiyoyatenda ni chukizo kubwa."

Endelea uk. 5



Madiba Mandela - Shujaa wa Afrika

Ziara ya Amir na Mbashiri Mkuu Dodoma na Singida

Na Mwl. Khalifa Jailani Amri, Manyoni Singida.

Katika siku chache zilizopita kiongozi mkuu wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya Tanzania Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry alifanya ziara katika mikoa ya Dodoma na Singida.

Amir na Mbashiri Mkuu alifika mkoani Singida akitokea Dodoma ambapo alifuatana na aliyekuwa Mbashiri wa mkoa wa Dodoma Maulana Sheikh Ghulam Murtaza pamoja na wajumbe wengine kadhaa. Katika mkoa wa Singida Amir na Mbashiri Mkuu alitembelea Jamat za Manyoni, Kinyeto na Kitumbili. Katika safari yake akiwa katika Jamaat ya Manyoni Amir sahib na Mbashiri Mkuu alikutana na wanajumuiyya wa hapo. Pamoja na mengi aliyozungumza pia aliwataka



Amir na Mbashiri Mkuu - Jamaat Ahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry

wanajumuiyya kwanza kuongeza juhudi ya maombi ya kumcha Mungu kiukweli sit u kwa ajili ya kupata radhi ya Mwenyezi Mungu pekee bali waweze kupata mafanikio

Endelea uk. 8

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

MAPINDUZI YA KIROHO

Neema yote hii kubwa unayoiona ya Waislam hivi leo kutembea kifua mbele huku wakionesha ubora na utukufu wa Qur'an Tukufu, rehema aliyoleta Mtukufu Mtume Muhammad (saw) na ufafanuzi wa kina wa aya za Qur'an Tukufu uliotolewa na mtumishi mnyenyekevu sana wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) unatokana na kutii maagizo ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) aliyesema; "Ikibidi tembeeni hata kwenye theruji kumfikia Masihi Aliyeahidiwa atakapo kuwa". Ni neema hiyo ambayo imetusaidia kuelewa vilivyo Qur'an Tukufu.

Neema zote tunazoziona ni za Allah ambaye hata bila kuombwa Ametutengenezea mahitaji yetu maji, hewa, jua, mwezi, mbingu, ardhi, n.k ni mapenzi makubwa yaliyoje na Allah pia ambaye tukifanya bidii kidogo Anatulipa kwa juhudi zetu. Kwa ufupi tunavuna tunachopanda.

Mwaka 2014 tudhamirie kwa dhati kupanda mbegu ya kumpenda na kumtii Allah kwani ni kwa kumpenda yeye ndipo tutapopata chimbuko la maendeleo ya jamii yetu. Ukifuta wazo la kwamba Allah Anakuona na kwamba kesho kuna malipo ndiyo mwanzo wa mtu kumtesa mwenzie, kumnyima haki yake, kumdharau, mwenendo ambao taratibu unaota mizizi katika taifa letu. Mateso yamezidi, uonevu umekithiri, kiburi kimeenea, majivuno yanavaliwa mithili ya shati. Tunahitaji tena kwa haraka sana mapinduzi ya kiroho. Kuwapenda majirani, kuwapatia haki hata maadui zetu, kusamehe na kusahau, kwa ufupi kama taifa tunatakiwa tuelekee kwa Muumba wetu. Ni kwa kuelekea kwa Allah ndipo tutapata utulivu wa kudumu.

Hisia za mtu ni kitu nyeti sana, ni muhimu kuheshimu hisia hizo. Na hakuna hisia iliyo kali ambayo imesababisha maafa katika sehemu nyingi za dunia kuliko dini. Cha ajabu ni kwamba Manabii wote wametoka kwa Mwenyezi Mungu na ujumbe wao siku zote umekuwa ni amani. Ni jambo la msingi kuelewa na kuheshimu dini ya mwingine. Na iwapo unatakiwa kufikisha ujumbe iwe ni kwa hekima na mawaidha mema. Siyo hisia za kidini tu, bali hisia za utamaduni na za historia ya mtu. Historia inatuonesha ya kwamba wote waliodharau hisia za wengine wamekumbwa na dhoruba ya kutoaminiana na kuheshimiana. Ndiyo maana katika Qur'an Tukufu tumeaswa kutotukana miungu wao wasije wakatutukania Mungu wetu wa kweli.

Ingawaje ugawaji wa rasilimali kwa haki na uadilifu ni jambo linaweza kuepusha kizaazaa katika nchi, ni lazima ikumbukwe ya kwamba masikini hawafanyiwi ihsani wanaposaidiwa, bali hiyo ni haki yao. Wanayo haki katika rasilimali ya nchi. Watu wachache kukusanya mali na wakaitumia wanavyotaka mara nyingine kwa mbwembwe na kebehi ni chimbuko la uhasama usio wa lazima. Uhasama huu unaweza kuepukika kwa kuwajali na kuwaheshimu wale walio masikini katika jamii.

Yote mazuri ya nchi yanaweza kupatikana kwa kumtegemea Allah na kwa kufuata njia Aliyotuonesha. Tukidiriki kwenda peke yetu tutakuwa kama ule mto katika methali moja ya kibantu ambayo inaeleza ya kwamba mto huo ulikwenda peke yake na hatimaye ukapotea. Tujiepushe utamaduni huo wa kwenda peke yetu. Tushikamane sote kwa kamba ya Mwenyezi Mungu. Mungu ibariki Tanzania.

Khalifa Mtukufu ahimiza mabadiliko ya kweli:

Kutoka uk. 1

wa fitina (kile kinachosababisha mapungufu hayo) haukukatwa basi baada muda mfupi tu tatazo hilo litajirejea tena.

Nilipoanza kufikiria mambo kwa mtazamo huu na kusoma zaidi, nimepata kuona upembuzi uliofanywa na Hazrat Musleh Maood (ra), juu ya jambo hili. Namna yake ya kuandika na kuongea juu ya mambo inao uzuri huu kwamba huweka swali mbele na kisha kulitolea majibu tena kwa njia ya mifano. Namna anavyotoa majibu kupitia nuru ya Qur'an tukufu, hadithi za mtukufu Mtume s.a.w. na maandidhi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. ni ya pekee na huwezi kupata mfano wake. Hivyo nimefikiria pia na leo tujipatie manufaa ya hotuba yake hiyo ambayo nitaieleza mbele yenu, sababu alizozieleza (kwa nini inakuwa vigumu kwa watu wengi kuleta mabadiliko ya kweli na ya kudumu ndani yao) ili nanyi muweze kufaidika na mwongozo wake alioutoa.

Alisema:
Miongoni mwa mambo yanayozikwamisha juhudi zetu za kuleta mabadiliko ya kweli ndani ya matendo ya mtu au yanatuathiri kwenye juhudi hizi: la kwanza kabisa kati ya hayo ni ile hisia au lile wazo kwamba makosa fulani ni madogo na makosa mengine ndio makubwa. Kwa maana nyingine wako watu ambao wenyewe wamejiamulia hivyo au wamefikia hapo kutokana na mafundisho ya viongozi wao wa dini. Wamefikia uamuzi kuwa makosa haya ni makubwa na haya ni madogo. Na jambo hili linakuwa kikwazo kikubwa kwao cha kuleta mabadiliko ya kweli na ya maana.

Matokeo ya dhana hizi ni mtu huwa sugu na kufikia hali ya uasi na ugumu wa moyo na kutokujali kufanya baadhi ya makosa huzalika na kupevuka ndani yake. Aina ya usugu wa mazoea ya kutenda dhambi na matendo maovu humea ndani ya nafsi ya mtu na ubaya wa maovu hayo hauonekani kuwa ni jambo kubwa na muhimu mbele ya makisio yao. Huanza kufikiria kwamba kutenda kosa fulani dogo si jambo lenye madhara au kwamba adhabu yake sio kubwa. Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema kwamba:
Kama mtu anapata ugonjwa, bila kujali kwamba ugonjwa wake ni mdogo au mkubwa, iwapo matibabu hayakupatikana kwa ajili ya ugonjwa wake huo na kama juhudi haifanyiki kupatikana kwa tiba ya ugonjwa huo basi mtu huyo hawezi kuwa mwenye afya imara. Doa au baka dogo jeusi linapotokeza kwenye uso wa mtu hupelekea mahangaiko na hofu ili lisije likakua na kuongezeka na hatimae kuuharibu uso wote wa mtu.Kunakuwanaainahiyohiyo ya baka jeusi iachwayo kwenye moyo wa mtu anayetenda kosa lolote. Kosa lidhaniwalo dogo hukua na kuwa kubwa pale mtu asipojali kuliondoa. Lile kosa dogo ndio lile baka dogo jeusi ambalo hatimae hukua na kuuathiri uso wote wa mtu liliyemdondokea.

Hivyo, tunatakiwa tushike hadhari na tusidhani kosa lolote kuwa ni dogo kwa sababu kufikiri kwa namna hiyo kunakuza dhana kwamba kosa hili ni kitu kidogo tu lakini kumbe mbegu ya kosa hili lililodhaniwa kuwa dogo hatimaye hukua na kusambaa na makosa hayo madogo baada ya kupita muda hugeuka na kuwa makosa makubwa kabisa. Hivyo kila mmoja wetu anatakiwa ajichunguze au ajitathmini mwenyewe kwa kutumia kigezo hiki.
Mwenyezi Mungu Mtukuka ameweka adhabu kwa kila kosa, liwe lidhaniwalo dogo au kubwa, Kisha tuangaliapo jinsi Mtukufu Mtume s.a.w. alivyofafanua kosa dogo na kubwa ni lipi na wema mdogo na mkubwa ni upi, tunagundua kwamba alitoa ufafanuzi tofauti kwa watu tofauti kulingana na tofauti za hali zao.
Katika mahala fulani alipoulizwa wema mkubwa ni upi alisema kuwatumikia au kuwahudumia wazazi ndio wema mkubwa. Lakini mtu mwingine alipomuuliza swali hilo hilo, ni lipi tendo jema zaidi alimwambia kwamba kuswali Sala ya tahajjud ndio wema mkubwa. Akimjibu mtu mwingine juu ya swali hilo hilo alimwambia kwako wewe wema mkubwa ni kwenda kupigana vita ya Jihadi. Hivyo inabainika wazi kwamba kwa watu tofauti wenye mazingira na hali tofauti tendo jema zaidi kwa ajili yao linakuwa pia tofauti
Wacha pia nizungumzie kidogo juu ya Jihadi kwani tunasingiziwa kwamba eti sisi hatushirikikwenyejihadi.Katika zama zile ambapo Uislamu ulikuwa ukishambuliwa kila upande kwa upanga, hivyo hivyo jihadi ya kutumia upanga ilikuwa ni tendo jema sana na yeyote ambaye alishindwa kushiriki bila ya sababu ya msingi alihesabiwa mbele ya Mwenyezi Mungu kuwa mwenye kustahiki adhabu. Lakini katika zama za Masihi Aliyeahidiwa a.s. Mtume s.a.w. alibashiri kwamba "Atazirejesha panga kwenye ala zake au kwa maana atasitisha vita za kidini kwa sababu njia na namna ya kuushambulia Uislamu itakuwa imebadilika. Islam kama imani haitoshambuliwa na adui kwa upanga, bali itashambuliwa kwa hoja na mantiki tena kwa kutumia njia za kileo za mawasiliano yanayowafikia watu wengi kwa wakati mmoja. Na hivyo Masihi Aliyeahidiwa a.s. na Jumuiya yake watatumia njia hizo hizo kujibu mashambulizi yatakayoletwa dhidi ya Uislam.
Kwa kuzingatia ukweli huo ndipo Masihi Aliyeahidiwa a,s, akasema katika moja ya ubeti wake kwamba: Kwa sasa kujiingiza kwenye vita vya kupigania na kuihami dini kumeharamishwa. Akimaanisha kwamba Jihadi ya upanga sio tu iliruhusiwa bali ilikuwa ni tendo jema sana katika zile zama ambapo adui alikamata upanga kwa ajili ya kuuangamiza Uislam. Lakini kwa sasa jambo hilo si wema tena, bali linageuka kuwa haramu hadi pale itakapofikia kwamba mtu fulani aanze kushika upanga kuiangamiza Islam, hadi pale itakapofikia mataifa yenye nguvu yashike silaha kwa ajili kuungamiza Uislam.

Sasa jambo linaloweza kutajwa kuwa ni wema mkubwa na aina ya jihadi inayotakiwa kufanywa ni kuyaeneza (kuyahubiri) mafundisho ya Islam, au jihadi ya kutumia elimu, jihadi ya kalamu, jihadi ya kueneza mafundisho ya Islam na uzuri wake tena kwa kutumia njia zile zile wanazozitumia wapinzani yaani kupitia vyombo na njia za kusambaza habari.

Iwapo mmoja wetu asishiriki kwenye jihadi hii kutokana na upungufu wake wa elimu, au kwa sababu nyingine yoyote, basi pia upo mlango wa yeye kushiriki kusambaza mafundisho ya Islam na uzuri wake na mlango huo ni kujitolea kwake kifedha ili kuwezesha hayo kufanyika. Lakini ieleweke pia kwamba yeyote awaye pamoja na kushiriki kwenye jihadi hii, lakini kama hatimizi wajibu wake alionao kwa mke wake na watoto wake au kwamba hashiki hadhari katika malezi yao basi kwa mtu huyo wema mkubwa sio jihadi hii bali kwanza ni kujitahidi kutimiza wajibu wake unaomkabili kwa familia yake. Na iwapo hatimizi

Endelea uk. 3

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Kutoka uk. 2

Khalifa Mtukufu ahimiza mabadiliko ya kweli:

Kutoka uk. 2

wajibu wake huo ipasavyo na hajali elimu yao na malezi yao ya kiroho basi mtu huyo anafanya kosa kubwa sana.

Katika zama za Mtukufu Mtume s.a.w. pamoja na amri ya kupigana jihadi, kama nilivyosema, alimwambia muislamu fulani kwamba kwake yeye wema mkubwa zaidi ni kuhudumia mzazi wake. Hivyo kwa kila mtu kutegemea na hali na mazingira yake, wema mkubwa na tendo jema zaidi kwake ni kitu tofauti na wengine.

Hivyo hivyo tunaona kwamba kukusanya mali kwa njia zisizo halali ni kosa kubwa na kumekatazwa. Lakini leo tunaona aina chungu mzima za mashine za kuchezesha kamari na njia mbali mbali za michezo ya kamari. Kuna watu wengi ambao wamesombwa na mchezo wa bahati nasibu na wengine hushinda kwenye mashine za kuchezesha kamari, ingawaje watu hawa katika hali ya kawaida ya maisha hawamuongopei yeyote, Hawapiti kiasi katika baadhi ya mambo wala hawamdhulumu au kumuua yeyote kwani wanadhania kwamba kufanya matendo hayo ni makosa makubwa. Lakini hawatafakari kwamba kucheza kamari na kupoteza mali nyingi kwenye upuuzi huo nalo pia ni kosa baya. Kwa watu kama hawa kupoteza hela zao kwenye kamari kunakuwa ni kosa kubwa kwao kwani angalau makosa mengine walishayaona kuwa ni makubwa kwa vyovyote.
Kisha tunawezakuwaonabaadhi ya akina dada ambao hawajali kujihifadhi na kuvaa vizuri (hijab) sawa na mafundisho ya Islam wanapokuwa nje ya majumba yao. Pamoja na kuwa kwake mama wa Kiahamdiyya hajali kufunika kichwa chake au hata kujitupia kitambaa cha kichwani. Pengine anavaa nguo zinazombana sana na kuonesha uzuri wa maungo yake, lakini utakapomueleza juu ya kujitolea kifedha, atafanya hivyo kwa moyo mweupe na pengine anachukia kutokuwa mwaminifu na anamchukia mtu anayeongopa mbele yake.

Hivyo kwa dada kama huyu tendo jema kwake sio kuzidi kuendelea kujitolea kifedha au kuzidi kusema ukweli, lakini kwake tenda jema zaidi kwa wakati huu ni kujitahidi kushikilia agizo la Qur'an tukufu linalomuelekeza juu ya kujihifadhi na kushika matakwa ya kuvaa hijab. Jambo lile ambalo analidharau na kuliona kuwa ni wema mdogo, ndilo jambo hilo hilo litakalomsukuma na kumtumbukiza kwenye kosa kubwa zaidi.

Hivyo itoshe tu kusema, kila tendo jema au baya lipimwe na



Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a)

lionwe kwa kutumia kigezo cha mtu binafsi mwenyewe sawa na hali yake na mazingira yake na matendo ya kila mtu yanaweza yakatoa tafsiri tofauti ya wema mkubwa au kosa kubwa kwa mtu huyo. Kwa vyovyote muda wote ambao mawazo haya yatabaki kwenye kichwa

cha mtu kwamba kosa hili na hili ni dogo na hili na hili ni kubwa au wema huu na huu ni mdogo na huu na huu ndio mkubwa, basi mtu huyo hawezi kamwe kujikinga na maovu na wala hawezi kupata Baraka ya kutumia nafasi ya kutenda wema.

Hivyo muda wote tuweke mbele yetu jambo hili kwamba kosa kubwa ni lile ambalo mtu anajikuta kuona shida kuliwacha na anajisikia ugumu kutengana nalo kwa kuwa limeshakuwa sehemu ya maisha yake. Na wema mkubwa kwa mtu ni lile jambo ambalo linamuwia vigumu kulitekeleza. Kwa maneno mengine makosa mengi ni makubwa kwa wengine na hayo hayo ni madogo kwa wengine, na hivyo hivyo wema mwingi ni mkubwa kwa wengine lakini huo huo ni kitu kidogo tu kwa wengine.

Hivyo iwapo kweli tunataka kuleta mabadiliko ya kweli na ya uhakika ndani yetu, basi kwanza ni lazima tuepukane na wazo hili bovu kwenye nyoyo zetu kwamba, labda kwa mfano kuzini ni kosa kubwa, kuua ni kosa kubwa, kuiba ni kosa kubwa, kusengenya ni kosa kubwa, lakini makosa yaliyobaki kwa kulinganishwa na hayo ya juu, ni vijikosa vidogo vidogo tu. Ni lazima tuzikinge nyoyo zetu na mawazo haya potofu.

Lakini pia hatuna budi tuzikinge nyoyo zetu na wazo hili pia kwamba kufunga saumu tu ndio wema mkubwa, au kutoa zaka tu ndio wema mkubwa, au kuhiji ndio wema mkubwa na wema mwingine uliobaki kwa kulinganishwa na matendo hayo ni wema mdogo mdogo – na hili ndio wazo linaloonekana kuwashika

Waislamu walio wengi. Iwapo mawazo haya hayatong'olewa kutoka kwenye nyoyo zetu, basi siku zote utendaji wetu utabaki kuwa dhaifu. Matendo yetu yataimarika pale ambapo tutaanza kushika nasaha za Masihi Aliyeahidiwa a.s. yaliyo mbele yetu kwamba "Yule ambaye hatekelezi amari zote 700 za Quran Tukufu anajifungia mwenyewe mlango wa wokovu.

Hivyo tusielewe kama wengine kwamba baadhi ya wema ni mdogo na mwingine ni mkubwa, kama wadhanivyo Waislamu wengine kwamba, kwa mfano, kufunga saumu ni wema mkubwa lakini hawaweki mkazo wowote kwenye kushiriki sala za jamaa.
Yule ambaye zaka inamuawajibikia atafanya kila njia kukwepa kulipa, lakini afikapo kwenye saumu atajitahidi kwa juhudi yake ya mwisho kufunga kwa sababu anahisi kwamba kama hakufunga atakuwa amefanya kosa kubwa kabisa.

Kutokulipa zaka wakati fulani (huko Pakistan) ilikuwa ni kesi – sielewi hali ikoje kwa sasa – hasa baada ya 1974 ambapo Waahmadiyya tukatangazwa kwamba sio Waislamu sawa na matakwa ya katiba ya Pakistan, hapo baadhi ya matajiri wasio Waahmadiyya walijiandikisha kwenye akaunti zao za benki kwamba wao eti ni Makadiani. Kwani Waislamu wote ilikuwa ni lazima wakatwe zaka moja kwa moja kutoka kwenye fedha zao zilizoko benki, lakini kwa vile Waahmadiyya walitangazwa kwamba sio Waislamu wao wakawa hawakatwi zaka, na hii ikawa ndio njia ya wengi wao kukwepa kulipa zaka.
Basi hii ndio hali ya imani yao, wanasema Waahmadiyya ni makafiri, lakini nafasi inapopatikana ya kuokoa fedha kwa kutokulipa zaka wanajitaja kuwa miongoni mwa wale waliokwisha watangaza kuwa makafiri. Sijui hali ikoje kwa sasa lakini hii ilikuwa ndio hali wakati fulani.
Na hali hii inafikiwa kwa sababu katika kuangalia lipi jema na lipi ovu hawajali muongozo wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake bali hufuata nyao za viongozi wao wa dini tu.

Hadhrat Muslehe Maud alieleza tukio moja katika maisha ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwamba katika mwezi mmoja wa Ramadhani wakati Masihi Aliyeahidiwa a.s. akiwa safarini kuelekea Amristar alipata nafasi ya kutoa hotuba. Wakati akitoa hotuba koo yake ilikauka sana na akaanza kukohoa, rafiki yake mmoja kwa kuona hali hiyo akampatia kikombe cha chai ili anywe lakini Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikataa. Baadae kidogo hali

ile ikarejea tena na rafiki yake yule akampatia tena kikombe ili alainishe koo lakini akakataa pia.
Lakini shida ile iliporejea tena kwa mara ya tatu na koo yake ikazidi kuwa kavu na rafiki yake akampatia tena kikombe, Masihi Aliyeahidiwa a.s. alichukua na kunywa kidogo akihofia kwamba wafuasi wake wasije wakaelewa kwamba anajionesha bure kwa kutokufaidika na amri ya mwenyezi Mungu inayowataka watu wasifunge wawapo safarini.
Lakini lo, kwa kuona hilo wasio waahmadiyya waliokuwepo hapo, wakapaza zogo kubwa wakisema angalia mtu huyu anajidai kuwa Mahdi kisha hafungi ndani ya mwezi wa Ramadhani.

Kwa mawazo ya watu hao, umuhimu wa kufunga saumu ni mkubwa kiasi hiki kwamba wako tayari kuendelea na saumu hata kama wanapingana na amri ya Mwenyezi Mungu. Hadhrta Muslehe Maud anasema kwamba kutoka kwenye kundi la watu wale yawezekana 90% hawajali hata kusali, na pengine 99% si wenye kushika ukweli na pengine wanashiriki kwenye njia za kudhulumu na kufanya njia zingine za ujanja ujanja wa kutafuta ulaji, lakini ni kweli kwamba kati yao 99% walikuwa wamefunga saumu kwa sababu wanadhani kwamba kufunga saumu ni wema mkubwa sana kuliko mwingine wote. Lakini hawafungi kama alivyoagiza Mtume s.a.w. kwamba yule anayefunga huku anasema uongo, au anasengenya au anawatukana wengine, saumu ya mtu huyo mbele ya mwenyezi Mungu si zaidi ya kushinda na njaa na kiu tu.
Kama tufanye uchunguzi, tutagundua kwamba wengi wa Waislamu wanashinda na njaa na kiu tu sawa na kipimo hiki cha Mtume s.a.w., Lakini kwa makisio yao kubaki huku na njaa na kiu ni wema mkubwa sana ambao unatosha kuwaokoa salama. Au wanaweza kuongeza matendo fulani madogo na kwa njia yao ya kufikiri wakadhani kwamba wametenda wema mkubwa wa kutosha kuwa maandalizi ya kupata msamaha wa Mwenyezi Mungu.

Watu kama hao hawawezi kamwe kusimamisha (kuonesha wema ni nini) duniani na pia hawawezi kufikia kiwango cha kuwaelimisha wengine hata waelewe ubaya (uovu) hasa ni kitu gani. Wamejiwekea vipimo vyao wenyewe vya wema mkubwa na wema mdogo mdogo na madhambi makubwa na madhambi madogo madogo na matokeo yake wanajaribu kufikia kile wanachokidhani kuwa ni wema mkubwa.
Na yale makosa wanayoyadhani kuwa ni madogo madogo hawajali wala hawajaribu kupambana nayo. Kule kutokuyaacha makosa hayo madogo ni ushahidi kwamba hawana nguvu ya kupambana nayo. Na hivyo wanaendelea kuzama zaidi na zaidi kwenye uovu kwa kufanya kosa moja baada ya jingine; wakati Uislamu hasa umeuita wema mkubwa lile tendo ambalo kwa kulifanya hilo mtu inabidi ajipinde na kujitahidi sana na hili linaweza likawa tofauti kwa kila mtu.
Na pia Uislamu umeliita kuwa ni kosa kubwa sana lile tendo ambalo mtu inamuwia vigumu sana kuachana nalo.
Hivyo, kama tunapenda tulete mabadiliko ya kweli ndani yetu, basi ni lazima tuliweke jambo hili mbele ya fikra zetu muda wote kwamba tutajaribu na kujitahidi muda wote kufanya kila tendo jema na wakati huo huo tutajaribu na kujitahidi kwa nguvu zetu zote kujiepusha na kila tendo ovu. Tafsiri za kujitungia sisi wenyewe tu, haziwezi kabisa kutufanya tutende wema hasa na tujiepushe na uovu wote. Mara nyingi mtu anajiletea madhara zaidi wakati anapoanza kujitungia tafsiri zake mwenyewe na kuamua ni ubaya gani wa kuuwacha na upi wa kuendelea nao na pia kuamua ni wema upi wa kufanya na upi wa kuuacha.

Wema ule ambao unaonekana mdogo kwa sababu ya kutokuujali hatimaye unamnyima mtu nafasi ya kutenda wema moja kwa moja,

Endelea uk. 4

Khalifa Mtukufu ahimiza mabadiliko ya kweli:

Kutoka uk. 3

na yale makosa ambayo kwa juu juu yanaonekana madogo, hayo hatimaye huleta madhara yasiyotibika juu ya maendeleo ya kiroho na utawa wa mtu mwishowe humzuia mtu kupata Baraka ya kupokea usafi na utawa kutoka kwa Mungu. Kisha kuna jambo hili pia kwamba mtu yule ambaye hajiepushi na kufanya makosa yote, mbegu ile ye kufanya uovu hubaki imara ndani yake na husubiria nafasi ipatikanapo tu iweze kuibuka na kuchanua na kuonesha makucha yake. Hadhari kubwa inatakiwa kushikwa juu ya hili.

Ili tupate mafanikio ya kuifanya tabia hii ya kutenda baadhi ya makosa ifutike moja kwa moja ndani yetu hatuna budi sote kwa pamoja tupambane kuifikia, tena sote kwa pamoja. Sisi tupo kwenye Jumuiya, na hitajio ni kwamba kila Mwanajumuiya ni lazima afanye juhudi.

Iwapo kila mmoja wetu anafanya juhudi kivyake kwa kutumia tafsiri yake ya wema na ubaya, basi mtu mmoja ataweza kufikiria jambo fulani kuwa uovu mkubwa sana na mwingine akafikiria jambo hilo hilo kuwa uovu mdogo tu na inawezekana mtu wa tatu akawa na wazo tofauti na hao wawili wa kwanza. Katika hali kama hiyo jamii kama Jumuiya haiwezi kamwe kuepukana na maovu.

Tutaweza tu kuyang'oa maovu yote ndani yetu iwapo sisi sote tutakuwa na fikra ya aina moja. Kwa mfano Waislamu wote wanauchukulia ulaji wa nyama ya nguruwe kuwa ni kosa kubwa sana kuliko hata kumshirikisha Mwenyezi Mungu. Kila mkosaji: awe mwizi, mzinifu, mnyang'anyi, mlevi, n.k anaweza kufanya hayo yote na bado akajihesabu kuwa Mwislamu, lakini kama utamwambia ale kipande kidogo tu cha nyama ya nguruwe atakujibu nitakulaje nyama ya nguruwe na hali mimi ni Muislam? Hujui kama mimi muislam, nitakulaje nyama ya nguruwe?

Sababu ya hali hii ni kuwa katika ulimwengu wa kiislamu ni kama wote wamekubaliana kwamba kula nyama ya nguruwe ni kosa kubwa na hakukubaliki kabisa. Pamoja na kuishi hapa na kuzaliwa kwenye jamii hii ya (Ulaya) na kukua hapa lakini Waislamu wanaoishi hapa asilimia 99% wanachukia sana na hawawezi kula nyama ya nguruwe. Hii inatokana na lile wazo au ile hisia ambayo imeendelea kukua miongoni mwa waislamu wote kama umma.

Hivyo ili tuweze kujiepusha na kila tendo ovu na ili tuweze kutenda na kukuza kila wema kuna haja ya lazima ya kumuamshakilamwanajumuiya aelewe na azingatie kwamba hata wema unaoonekana mdogo kiasi gani basi huo ni wema mkubwa sana na hata ule uovu unaoonekana kuwa mdogo kiasi gani basi huo ni uovu mkubwa sana. Hadi pale ambapo fikra hizi zitakuwa kwenye mawazo ya kila mmoja wetu, na iwapo juhudi hazikufanywa ili kuleta mabadiliko hayo, makosa mbalimbali yataendelea kuonekana ndani ya mwanajumuiya huyu na yule na jambo hili litaendelea kuwa kikwazo kikubwa cha kuleta mabadiliko ya kweli kati yetu.

Sababu ya pili inayokwamisha kuleta mabadiliko ya kweli ni mazingira na tabia ya kuiga mambo kwa wengine. Mwenyezi Mungu Ameweka sifa hii ya kuiga kwa wengine ndani ya silika ya mwanadamu na jambo hili hujionesha tangu utoto wetu. Na hili limefanywa kuwa sehemu ya silika zetu za asili bila shaka kwa ajili ya manufaa yetu, lakini hata hivyo matumizi mabaya ya sifa hii badhi ya nyakati humpelekea mtu kwenye maangamizi.

Ni kutokana na sifa hii ya kuiga na kuathiriwa na mazingira ambayo humpelekea mtoto aige lugha kutoka kwa wazazi wake na kujifunza mambo kadhaa, mazuri ambayo kwa kujifunza hayo mtoto hukuwa akiwa na tabia njema.

Iwapo wazazi ni watu wema na wanaichunga Sala vizuri na wanasoma Qur'an na wanaishi kwenye mazingira ya kupendana na kuhurumiana kila mmoja na wanachukia na kujitenga na uongo, basi na watoto walio chini ya uangalizi wao, nao pia watakuwa wenye kuiga mazuri hayo.

Lakini kinyume chake iwapo wazazi na wenye kuishi kwa kuongopa, kugombana na kupigana, mazungumzo ya matusi nyumbani pamoja na kuwadharau na kuwadhalilisha wengine, iwapo hawajali heshima na nidhamu ya Jamaat, na mambo mengine mengi mabaya, wakati watoto wao wakiyaona hayo, basi kutokana na tabia ya kuiga au kutokana na hali ya kuathiriwa na mazingira, watoto pia wataiga mambo haya mabaya.

Mtoto aendapo nje kila akionacho kwenye mazingira yaliyomzunguka, kwa marafiki zake, huiga mambo hayo pia. Hii ndio sababu mara kadhaa nimewakumbusha wazazi waangalie sana mazingira ya nje yanayowazunguka watoto wao. Bali hata ndani ya majumba, vipindi mbali mbali vinavyoangaliwa kwenye luninga (TV) au kupitia mtandao hivyo pia vikaguliwe kwa umakini.

Na hili pia ni jambo muhimu kueleweka kwamba umri wa kujifunza wa mtoto unaanzia tangu miaka yake ya mwanzoni kabisa. Jambo hili likumbukwe daima na litiliwe maanani. Wazo hili lisipite kwenye akili zetu kwamba tusubirie watoto wetu wawe wakubwa kisha ndipo tuanze kuwafunza. Umri wa miaka 2 hadi 3 ni umri tosha kwa mtoto kuanzishwa mafunzo fulani. Kama nilivyosema mtoto huwaangalia na kujifunza kutoka kwa wazazi na wale walio wakubwa ndani ya nyumba na kuanza kuwaiga. Wazazi wasifikiri wakati wowote kwamba watoto bado ni wadogo, na kwamba hawajui chochote. Kwa kweli mtoto anajua kila kitu, na anakichunguza kila kitendo kifanywacho na wazazi, na matendo ya wazazi huacha athari moja kwa moja kwenye ubongo wake bila ya hata kukusudia. Na muda ufikapo naye huanza kuigiza matendo hayo.

Mabinti, kwa namna ya pekee huwaigiza mama zao, na wakati wakicheza michezo yao huanza kuigiza jinsi mama zao wanavyovaa. Wavulana nao huanza kuwaigiza baba zao. Mazuri na mabaya ambayo wazazi wanayafanya wanaanza kuyaiga. Kwa mfano wanapokuwa wakubwa na kuanza kuelezwa kwamba jambo hili ni baya na hili ndilo zuri, kusema uongo kwa mfano ni jambo baya na kutimiza ahadi ni jambo jema. Lakini mtoto yule ambaye hakuwahipo kumuona mzazi wake akitimiza tendo jema la kusema ukweli, au iwapo hakuwahipo kuwaona wazazi wake wakitimiza ahadi zao, mtoto huyo atayaelewa mambo hivi kwamba ingawaje kusema uongo na kutokutimiza ahadi sawa na misingi ya kielimu ni jambo baya, na mtu kutimiza ahadi zake ni jambo jema, lakini hawawezi kuiingiza elimu hiyo kwenye matendo, kwa sababu hiyo ndiyo hali waliyoendelea kuiona nyumbani mwao, kwamba watu wanaishi kinyume na hayo yote. Watoto huanza kujipanga kwenye hali hizo na wakuapo zaidi hupata usugu wa kutokukubali chochote.

Iwapo mtoto anamuona mama yake akiwa mvivu kwenye kutekelaza ibada ya sala, na baba arudipo nyumbani akimuuliza iwapo amesali au la, mama hujibu 'sijasali lakini nitasali sasa hivi', mtoto hudhani kwamba hilo ni jibu kubwa. Kwamba mtu yeyote akinuliza kwamba nimesali au la nami pia nitajibu hivyo hivyo, sijasali, lakini nitasali sasa hivi. Au mtoto akisikia jawabu kutoka kwa mama, 'nilisahau', au iwapo mama atasema nimesali na hali mtoto alikuwa na mama yake kutwa mzima na hajamuona akisali, basi mtoto pia naye atasajili majibu hayo kwenye kichwa chake.

Hivyo hivyo matendo mabaya ya baba pia hubakisha athari ya kudumu kwenye akili ya mtoto na jibu lolote baya mbalo baba analitoa basi mtoto atalisajili akilini mwake hilo pia. Hivyo basi, wote mama na baba, kuhusiana na malezi ya mtoto, iwapo wanafanya makosa au wanafanya matendo machafu basi wanamuongoza mtoto wao kwenye njia isiyo sahihi na wanabakisha kichwani mwake elimu isiyo sahihi kutokana na matendo yao. Na mtoto akuapo atafanya kama walivyofanya wazazi wake.

Hivyo hivyo matendo mabaya ya majirani na marafiki wa wazazi nayo pia hubakisha athari mbaya sana kwa watoto. Basi iwapo kweli tunataka tulete mabadiliko na mageuko ya kweli kwenye kizazi chetu kijacho na watoto wetu na ili kwamba kiwango cha kujitengeneza kwetu kiwe kikubwa, basi wazazi hawana budi wawe makini na mazingira yao na kila tendo lao walitendalo, na pia wawe na urafiki na watu wale tu ambao ni wema na walio sawa na utendaji wao. Hivyo basi tabia ya kuiga tangu utotoni na athari iletwayo na mazingira ni mambo yabakishayo athari kubwa kwa mtoto. Iwapo utamuweka mtoto kwenye mazingira mema basi naye ataanza kutenda mema na iwapo utamuacha mtoto kwenye mazingira machafu na mabaya naye pia ataanza kutenda mambo mabaya. Na wakati mtoto aliyekwisha iga kutenda mambo mabaya, akuwapo na kujaribu kumuelimisha kwamba jambo hili na hili ni baya na hivyo usilifanye, kwa wakati huo anakuwa amefikia kiwango cha kutokukunjika tena na wazazi katika nyakati hizo tena hawana haki ya kulalamika kwamba watoto wetu wamekuwa wabaya.

Hivyo basi, hili ni jukumu na wajibu mkubwa sana wa wazazi, kwamba, kupitia matendo yao wawafanye watoto wao wawe wenye kusimamisha sala. Kupitia matendo yao, wawafanye watoto wao wasimame juu ya ukweli. Na kwa kupitia matendo yao wawaimarishe watoto wao kwenye sifa na matendo mengine mema ili nao pia waweze kuigiza sifa na matendo hayo. Wazazi wajiepusha na kuapa viapo vya uongo ili kwamba na watoto pia nao wakingwe dhidi ya tabia hiyo chafu.

Ni kiwango gani cha athari ibakiayo kwenye matendo ya mtoto kutoka kwa wazazi wake, inaweza kupimwa kutoka kwenye mfano huu wa mmoja wa Masahaba wa Masihi aliyeahidiwa a.s. ambao Hadhrat Musleh Mauud ameutoa. Sahaba huyu alitokea kwenye Usingasinga na kusilimu. Alikuwa hajawahipo kula nyama ya ng'ombe. Lakini rafiki zake wakawa wanamdhihaki kwamba hayo ni mambo yaliyokwisha pita, maadamu wewe umeshasilimu inakubidi ule nyama ya ng'ombe. Hazrat Musleh Mauud anasema siku moja aliwahi kumuoona sahaba huyo akitembea kwa haraka kuwakimbia rafiki zake maeneo ya nyumba ya wageni kwa sababu tu rafiki hao walikuwa wanasisitiza kwamba leo tutakufanya ule kipande cha nyama ya ng'ombe. Naye alikuwa akiwaomba kwa kuwabembeleza kwamba wasijaribu kumlazimisha kufanya hivyo. Na iliwahi kusemwa kwamba mara walipofanikiwa kumlazimisha kula kipande hicho cha nyama ya ng'ombe, sahaba yule alianza kupata homa kali na hatimaye kutapika.

Basi, haya yalikuwa ni matokeo ya hali iliyopevuka kwa sahaba huyu ya kuchukia sana kula nyama ya ng'mbe, tabia aliyoirithi tangu utotoni kutoka kwa wazazi wake. Na hivyo baada ya kukua na hata baada ya kuukubali Uislamu hali hiyo ya kuchukia kula nyama ya ng'ombe bado iliendelea kugandamana naye. Bila shaka alikuwa amebadili imani na kukubali mafundisho yote ya imani yake mpya lakini kuchukia kule ambako wazazi wake walimrithisha kutokana na matendo yao hakukuweza kubadilishwa.

Hazrat Musleh Maood (ra) anasema kwamba matendo, kwa vile yanaweza kuonwa, watu wanaweza kuyaiga haraka na baadae mbegu ile inaendelea kukua, lakini imani si kitu kinachoweza kuonekana, na hivyo inabaki kwenye mipaka maalum tu. Mfano wa imani ni kama mfano wa kupadikiza mti kwa kuachanisha vitawi vyake na kupandikiza pengine wakati mfano wa matendo ni kama kupandikiza mti kwa kutumia mbegu. Mbegu huota kwa kupandwa ardhini na inaanza kuchipua yenyewe muda wowote mazingira yatakaporuhusu.

Hivyo ni rahisi sana kwa matendo mabaya kupandikizwa na kuenezwa. Na hayo huenezwa haraka kwenye jamii kutokana na matendo maovu ya wetu wenyewe na pia kutokana na matendo mabaya ya watu wa nje. Hivyo kuna nafasi kubwa ya jamii katika kueneza mabaya au mema. Basi muda wote tuyaweke haya akilini mwetu. Kuna sababu zingine pia, ambazo Inshallah nitazieleza kwenye hotuba zijazo.

Mwenyezi Mungu Atujaalie siku zote kuweka fikra zetu vyema na kushughulika na kuzitengeneza hali zetu na za watoto wetu. Amin.

Kazi ya kuitangaza Islam ni ya Ahmadiyya pekee - Asema Khalifa Mtukufu a.t.b.a.

Na Dawati la Kiswahili
Morogoro

Kutoka Toleo lililopita:

Wenye mamlaka wameelezwa mwanzoni kwamba wafanye uadilifu, nao pia kama hawatekelezi wajibu wao, na hawajitolei kwa wakati unaotakiwa kwa ajili ya kazi za Jamaat, hawafanyi maamuzi kwa kutafakari, hawafanyi uadilifu kwa wanajamaat katika mambo yao, basi watawajibika mbele ya Allah Taalah.

Ama mwanajumuiyya wa kwaida naye anawajibu na faradhi juu yake anayotakiwa kuitekeleza,pia nimekwishaeleza kwamba kama hafanyi juhudi kwa ajili ya kutekeleza ahadi yake ya baiat, basi ataulizwa na Mwenyezi Mungu.

Kisha kuna ahadi muhimu sana ninayotaka kuwakumbusheni, nayo ni ile inayofanywa na kila mwananchi kwa ajili ya Allah au Qur'an au pengine kwa jina la mfalme wa nchi husika, hiyo pia inatakiwa kutekelezwa na kuzingatiwa na kila Mwislamu, na kutoitekeleza ni upungufu wa imani.

Mtume s.a.w. anasema: kuipenda nchi ni sehemu ya imani. wanajumuiyya wanatakiwa kuitafakari kwa undani kabisa. Ninayo taarifa kuwa baadhi ya wanajumuiyya, wakati mwingine wanapofanya biashara, huwaajiri watu na kuwapa ujira mdogo, au wanaonesha ujira mdogo ili wadai manufaa mengine kutoka kwa Council (serikali wa mji), na wanawaambia kwamba haya tunayafanya kwa ajili ya faida yenu, lakini wao wenyewe wanasema uwongo na kuwalazimisha wengine pia kusema uwongo, hawatekelezi ahadi yao na huwahimiza wengine kutoitekeleza,kwa kufanya hivyo wanajipatia faida.

Watu wa aina hii, juu ya mapato yao na pesa zao, wanajaribu kutolipa kodi ya serikali,ambapo ni hasara kwa serikali na kwa kutoitekeleza ahadi yao, kisha kwa kuwapa wafanya kazi wao ujira mdogo, badala ya kuwatumia sawasawa na kuwasaidia ili wapate posho kutoka serikalini,wanaitia hasara hazina ya Taifa.

Basi hizi zote ni dhulma tupu na uvunjaji wa ahadi ile aliyoifanya wakati wa kupata uraia,hii ni sawa sawa na kuivunja ahadi ya Bai'at, kwani ni lazima kusema kweli, hivyo hawa wanavunja ahadi ya serikali na ya Jamaat na kutenda dhambi. Hivyo kila mwanajumuiyya anapaswa kujichunguza pande zote.

Kisha nataka kueleza juu ya ubaya mwingine ambao unaziharibu nyumba zingine na kuondoa utulivu wa familia zingine. Huo ni kutokufuata amri ya Allah wakati wa kutoa Talaqa au wakati wa kudai Talaka, na kuivunja ahadi yake, uadilifu na kusema kweli, katika udugu huu umeshaelezwa mapema, na kama tunaufuata (ukweli na uadilifu) basi matatizo hayatazalika au yatasuluhika, lakini baada ya kupatikana kwa tatizo au kutokuelewana baina ya mume na mke, basi nasaha iliyotolewa na Allah izingatiwe, hususan mume, aishike vizuri,

Allah Talah anasema: "Kama mkitaka kubadilisha mke badala ya mke mwingine,na mkishampa mmoja wao rundo la mali, basi msichukue hata kidogo katika hilo, je, mtaipokea kwa kusingizia au kwa kutenda dhambi kubwa, na mtaipokeaje hali wameshachukua ahadi madhubuti ya kuishi pamoja kutoka kwenu.

Kama mafundisho haya yashikiliwe vizuri na yazingatiwe basi, kesi ambazo zinaendeshwa kwa muda mrefu katika nchi zetu,zisingechelewa kwenye mahakama husika, yaani Qadhaa.

Baadhi ya watu huwasingizia wanawake baada ya kuwapa Talaka,hiyo ni dhambi iliyo wazi kabisa,hata kama kuna la uhakika la kusema, hata hivyo tuliache kwa ajili ya Allah,kwani kuna masharti mengi kwa ajili ya mashahidi.

Jambo la pili ambalo ni muhimu ni kwamba Ndoa ni ahadi. Na mume na mke wanafunga ahadi baina yao,Allah Taalah anasema, ahadi hizo za siri pia zitekelezwe hata kama hakuna shahidi, mtekeleze yale yote yaliyofanyika baina yenu hata kama mnaachana, kwani Mungu Yupo popote na muda wowote, na msiombe kuzirudisha zawadi zile mlizoishazitoa, mume anatakiwa kutoa mahari katika kila hali, isipokuwa kama hakimu anatoa amri kwa kuyaona makosa makubwa ya mke. Hizi ni hila tu kwamba mahari haitolewi wakati wa Talaka inapodaiwa na mke, haya hayahusiani na haki za mke, hila za aina hii hazitakiwi, haya yanamaelezo mengi lakini saa hizi napenda kuwaelezeni kwamba, mkumbuke kuwa ndoa ni ahadi, inayotakiwa kuitekeleza katika kila hali, na kama kwa bahati mbaya inalazimika kuivunja ahadi hii, basi inatakiwa kuzingatia baadhi ya mambo ya muhimu na kuhifadhi siri za mwingine.

Ndani ya amri hii, kama mwanamke amepewa haki za usawa, basi yeye pia analazimika kutekeleza ahadi hii, akishikamana na uadilifu na ukweli, na kutekeleza wajibu wake wa nyumbani, na kama akiona tatizo, asimsingizie mume wake bila ya kuwa na sababu ya msingi.

Sayyidna Ahmad a.s. anasema akieleza kiwango cha Mwaminio kinachotakiwa kipatikane kwake anasema:

Waaminio ambao huyazingatia mambo yao yenye kumhusu Mungu au viumbe vyake, na hawawi wavivu katika kuyatekeleza, bali wanakuwa na hofu ya kwamba, wasiwe chini ya lawama yo yote, mbele ya Mola wao, huzingatia zaidi ahadi yao na amana zao, na kila wakati wanajichunguza kulingana na amana zao na ahadi yao, na wanazichungulia kwa darubini ya taqwa ili isije ikatokea upungufu katika amana zao na katika ahadi yao, na amana ambazo ziko kwao kutoka kwa Allah, kama vile nguvu zao za kimaumbile, sehemu yote ya mwili, heshima, na mali n.k. huzitumia kwenye mahali pao kwa uangalifu na kwa ucha-Mungu, na ahadi waliyoifanya na Mwenyezi Mungu wakati wa kuamini, hujitahidi kuitekeleza kwa kuzitumia nguvu zao zote, na kwa ukweli wote.

Vivyo hivyo amana za watu ambazo ziko kwao, au vitu vingine ambavyo vinakuwa kama amana, wanazitunza sawa na uwezo wao, na kama ukitokea ugomvi, basi hutoa amri kwa Taqwa, hata kama wanajipatia hasara kwenye amri hii. Njia zote za taqwa, ambazo ni nyembamba sana, huzingatiwa katika mambo yao yote, uzuri kamili wa kiroho kwa mwandamu ni katika kushika njia zote za ucha-Mungu.

Njia nyembamba za Taqwa ni naqshi latifu za uzuri wa roho na sura yake inayopendeza, na ni wazi kabisa kwamba kuzingatia ahadi na amana za Allah, na sehemu zote za mwili ambazo, kidhahiri, ni macho, pua, masikio, mikono, miguu n.k. na kindani ni moyo, nguvu zingine na khulka, kisha kuzitumia hizi zote vizuri sawa na uwezo wote, katika wakati wake, na kuzizuia kutoka mahali pasipojuzu, na kushika tahadhari kutokana na mashambuio yao ya siri.

Na kuzingatia haki za wanadamu wengine pia, ndio njia ya msingi ya uzuri kamili ya kiroho ya binadamu, na Mwenyezi Mungu Ameitaja taqwa kuwa ni mavazi ndani ya Qurani Tukufu, hivyo mavazi ya taqwa ni neno la Qur'an Tukufu, hii inaashiria kuwa, uzuri wa roho na mapambo yake, huzaliwa na taqwa. Na taqwa ni hii kwamba, mtu azingatie amana zote za Allah na ahadi yote ya imani pamoja na kuzingatia amana na haki zote za wanadamu wengine, yaani atekeleze hizo zote kwa undani kabisa sawa na uwezo wake.

Mwenyezi Mungu Atujaalie kufuata maamrisho ya Allah tukuzingatia taqwa,na tutekeleze ahadi zetu zote, na juhudi tulizofanya huko nyuma. Tushikamane nazo mbele, kwa kusali Ijumaa ya leo,iliyo ni ya mwisho wa ramadhani, na kufaya mema ndani yake, tusidhani kwamba haya yanatosha, na tusiya ache haya yote, bali kama Mwenyezi Mungu amevyosema: Muumini ni Yule ambaye anadumu katika wema wake, na kutekeleza ahadi zake.

Mwenyezi Mungu Atujaalie baraka nyingi kutokana na Ramadhani hii, na maamrisho ya Allah yaliyoandikwa ndani ya Qur'an Tukufu, tuyaelewe zaidi kuliko awali.

Nimeeleza baadhi ya mifano ya maamrisho ya Allah ili kila mmoja wetu awe na tabia ya kuyatafuta ndipo tutaweza kujihesabu miongoni mwa wale waliojifaidisha kwa Ramadhani.

Mwenyezi Mungu Atujaalie wengi wetu wawe waliojifaidisha nafsi zao, na waendelee kujifaidisha milele. Amin.

Somo Kutoka Pretoria

Kutoka uk. 1

Mandela aliamini katika Demokrasia na makamu wake akawa Fredrick de Clerk mzungu kindakindaki na kiongozi wa ubaguzi wa rangi Afrika ya Kusini. Uvumilivu, kusema na kutenda hizo ni dalili za muungwana Mandela. Na wa kumshinda katika hilo kwenye siasa za Afrika simfahamu. Labda unisaidie! Hata hivyo sikukata tamaa niliendelea kutafakari na hatimaye nikapata mambo mawili ambayo ni hazina kubwa kwa bara la Afrika na dunia kwa ujumla. *Umuhimu wa historia, mizizi yetu tulikotoka na umahiri wa kujenga hoja*.

Kwa kiwango kikubwa sisi katika Afrika tumeacha utamaduni wa kuwaweka kitako watoto wetu na kueleza utajiri wa historia za mashujaa wetu waliosimama kidete na kupambana ili kulinda heshima yetu. Bila hivyo tutawezaje kujenga uzalendo, mahaba ya utu wetu na ushujaa wa akina Asikia, Samora Ture, Shaka, Lobengura, Dedan Kimathi kwa kuwataja wachache tu. Jambo hili ni la msingi sana kwani linafanikiwa katika kumkunja samaki angali mbichi. Hatukatai ya kwamba kumfahamu Nepolion na Alexander si vibaya lakini kama wasemavyo ukarimu huanza nyumbani. Tunao wajibu mkubwa wa kuwafahamu mashujaa wetu akina Mkwawa, Kinjekitile Ngwale, na wengineo wengi.

Madiba Mandela katika kesi yake ile maarufu ya 1964 anaeleza kinaga ubaga na kutoa shukrani kubwa kwa wazee wa Transky ambao walikuwa na desturi ya kueleza vijana historia ya mashujaa wao. Akina Dingane, Bambata, Hintsa na Makana wengine ni Squngthi na Dalasile, wengine ni Moshoeshoe na Sekhukhuni. Mashujaa hao walipigania heshima ya Afrika, adha ya kutawaliwa na kunyanyaswa. Ni maelezo haya yaliyojenga mbegu katika moyo wa Madiba wa kudhamiria kwa dhati kupata fursa ya kutetea na kulinda heshima ya Afrika kama walivyofanya mashujaa hao wa Afrika ambao walijibu vizuri swali la Shaaban Robert; 'Je ni heri kufa kwa sondo au kufa kwa kondo?' Hao waliamua kufa kwa kondo. Kwa kufuata nyayo zao Mandela nae akaamua heri kufa kwa kondo na ndiyo maana katika neno lake la mwisho katika utetezi wake katika ile kesi maarufu iliyoitwa ya ugaidi Aprili 1964 hakuuma maneno alisema bayana niko tayari kufa.

Swali tunajiuliza Madiba angepata wapi taswira ya mateso waliyoyapata mababu zetu hadi wakaamua kupambana. Kama tulivyokwisha sema samaki daima hukunjwa angali mbichi. Madiba alitengenezwa vilivyo akawekwa sawa, akapewa maelekezo yakamtua akilini na usione vyaelea vimeundwa. Hatujui kama Mandela angepatikana bila ya mababu hao ambao walifufua fahari ya Afrika na kumuonesha ya kwamba heshima inapatikana kwa kujibu kiburi kwa kiburi. Tunajiuliza utamaduni huu wa kueleza vijana wetu heshima za mashujaa wetu tunaundeleza? Je hatukuzama katika uzungu, usiofiga wala chungu? Maisha ya Mandela yanatukumbusha Waafrika tuchukue zaidi katika historia yetu na tuhakikishe historia hiyo maridhawa inatunzwa na kuenziwa na kuwapatia vizazi vijavyo historia hiyo iliyotukuka. Maisha ya shujaa Mandela ni ushahidi wa umuhimu wa kueneza, kuenzi na kutekeleza kwa vitendo historia yetu.

Tusipochukua tahadhari kubwa maisha yetu yote yanaweza kuharibiwa au kutengenezwa na yale yanayotusibu. Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kwa miaka 13 aliteswa katika bonde la Makka. Hayo yalikuwa ni

Endelea uk. 6

Bustani ya Washairi

Mmatumbi asilia ameibuka tena na mistari inayoiombea dua Duthumi na wale walioga dunia.

1 Bismillahi kianzo, kwa jina alotuumba
Mwenye sifa njema nazo, waja kwake tunaomba
Tuyaache makatazo, ya Mola yasende demba
Duthumi iangazie, mwanga ulojaa nuru

2 Duthumi iangazie, mwanga ulojaa nuru
Twaomba utukidhie, twaomba Mola nusuru
Ulinzi utupatie, Ee Rabbana tunusuru
Duthumi iangazie, mwanga ulojaa nuru

3 Wapo walioanzia, Duthumi yetu Jamati
Sasa wametangulia, maisha yao tamati
Nasi tulio bakia, tuongoze mikakati
Duthumi iangazie, mwanga ulojaa nuru

4 Mola uwalaze pema, baba na mababu zetu
Wameondoka mapema, ndani ya Jamati yetu
Dunia si lelemama, ndanimwe hatuna yetu
Duthumi iangazie, mwanga ulojaa nuru

5 Sote tulio bakia, tukae na kushukuru
Tutii kwa kusikia, waingie msururu
Tabu shida, vumilia, mola atatunusuru
Duthumi iangazie, mwanga ulojaa nuru

6 Tuombe kwake Rabuka, tuombe bila kuchoka
Na njia ilonyooka, waja tupate ishika
Neema za Mola kushuka, ndogo kubwa kufurika
Duthumi iangazie, mwanga ulojaa nuru

7 Tamati natamatia, mwisho ninaashilia
Rabbi afungue njia, baraka kutushushia
Tunakuomba jalia, maombi yetu sikia
Duthumi iangazie, mwanga ulojaa nuru

Bi. Muhaymina Hamidu (Mmatumbi Asilia)
Duthumi - Morogoro.

Kuna mambo mengi ambayo humsukuma Mshairi kutunga. Al-Ustadh Khamisi Sultani Wamwera anafafanua msukumo unaomsukuma kuingia katika bahari hii ya ushairi.

1 Sijakuwa sawa sawa, kwa lugha lahaja sina
Bado ninasumbuliwa, ufasaha wa kunena
Nahau sijaijuwa, falsafa na maana
Ni kwa kuelimishana, situngi kwa kusifiwa.

2 Mantwiki sijaijuwa, urariri washindikana
Mizani hupungukiwa, sivipangi vyema vina
Nahisi nawachefuwa, mabingwa wanapoona
Ni kwa kuelimishana, situngi kwa kusifiwa.

3 Utunzi ama kipawa, mgawaji Maulana
Wa leo wamegawiwa, mithili wale wa jana.
Allah nami ningepewa, ningelishukuru sana
Ni kwa kuelimishana, situngi kwa kusifiwa.

Utoaji wa mali ni jambo la msingi na ni la lazima, kwa hakika kila kitu kinahitaji mali. Kama alivyosema Shaaban Robert 'pepo nayo yahitaji mali'. Al-Ustadhi Khamisi Sultani Shamte Wamwera anatukumbusha juu ya jambo hilo.

1 Anayo nyumba ya mawe, ana gari za serera
Ana mashamba kongowe, na duka za biashara
Anafuga na wenziwe, ng'ombe mbuzi na sungura
Kutoa kwa mali kwa Allah, kumekuwa mtihani

2 Kwa umbo na taswira, si kama mimi na wewe
Wajihi wake wang'ara, umestawi mwiliwe
Akivaa wastara, ni yeye atambuliwe
Kutoa kwa mali kwa Allah, kumekuwa mtihani

3 Afadhali na ajuwe, neema hiyo fundira
Amepewa na Molawe, si akili si busara
Akakumbuka atowe, fungu la Mola Kahara
Kutoa kwa mali kwa Allah, kumekuwa mtihani

4 Mliokuwa vinara, vizuri ashituliwe
Pia ingekuwa bora, waraka waandikiwe
Hali iliyomdara, si njema na aombewe
Kutoa kwa mali kwa Allah, kumekuwa mtihani

LIFAALO BINADAMU

1 Mawazo yanayodumu, siyo yako Mwenyekiti
Bileshi wajidhulumu, mzima kesho mauti
Ya kudumu yakarimu, ndiyo yenye ithibati
Lifaalo binadamu, ndiyo hasa la kudumu

2 Yale ndiyo ya dawamu, alopitisha idhati
Siyo wewe binadamu, haihati haihati
Wewe mwana wa Adamu, saghiri kama kijiti
Lifaalo binadamu, ndiyo hasa la kudumu

3 Ishufu hiyo rasimu, imeleta sharubati
Tatu sasa si haramu, huwezi pigwa manati
Bendera tatu zitimu, ziwe kwenye milingoti
Lifaalo binadamu, ndiyo hasa la kudumu

4 Mushawara ni muhimu, bora pia hasanati
Tena usiwe mgumu, mithili fupa la nyati
Ukishindwa siyo timu, andisi na uzatiti
Lifaalo binadamu, ndiyo hasa la kudumu

5 Kila kitu kina zamu, tena kinao wakati
Likisha lako jukumu, zaja nyingine nyakati
Kupinga hilo vigumu, kinyume cha harakati
Lifaalo binadamu, ndiyo hasa la kudumu

6 Kaditamati nujumu, kungarisha samawati
Mara hupita hukumu, kupungua thamarati
Ipo pia jahanamu, nayo naimu jannati
Lifaalo binadamu, ndiyo hasa la kudumu

Mahmood Hamsin Muhiru (Wamamba)
Dar es salaam

KUTOA MALI
Anayo nyumba ya mawe, ana gari za selera
Ana mashamba Kongowe, na duka za biashara
Anafuga na wenziwe, ng'ombe, mbuzi na sungura
Kutoa mali kwa Allah, kumekuwa mtihani!

Kwa umbo na taswira, si kama mimi na wewe
Wajihi wake wang'ara, umestawi mwiliwe

Akivaa wastara, ni yeye atambuliwe
Kutoa mali kwa Allah, kumekuwa mtihani!

Afadhali na ajuwe, neema hiyo fundira
Amepewa na Molawe, si akili si busara
Akakumbuka atowe, fungu la Mola Qahara
Kutoa mali kwa Allah, kumekuwa mtihani!

Mliokuwa vinara, vizuri asituliwe
Piya ingekuwa bora, waraka aandikiwe
Hali iliyomdara, si njema na aombewe
Kutoa mali kwa Allah, kumekuwa mtihani!

Al – Ustadh Khamisi S.S. Wamwera
Kimbangulile – Mbagala Rangi tatu - Dar es salaam

WEMA NA MAHALI PAKE
Tuseme tujibizane, kwa hoja na buruhani
Na jawabu zipatane, na kila swali betini
Maneno yasivungane, upendeze ukinzani
Wema umejibu nini, hoja ya beti ya pili?

Kwamba kilimo ni wema, ulimapo rutubani
Humeeshi na kuchuma, wendapo lima jangwani
Hoja hii muhakama, unaipa jibu gani?
Wema umejibu nini, hoja ya beti ya tatu?

Kwamba kusadi ni wema, si kusadi mahaini
Kusaidia dhuluma, ni jinai sheriani
Sipo mahali pa wema, kufanya hivi jamani
Wema umejibu nini, hoja ya beti ya nne?

Kwamba ibada ni njema, kwa majira muayani
Neno zuri kuparama, kwa ambaye afukani
Pofu kutosifu wema, ni kwa sababu haoni
Wema umejibu nini, hoja ya beti ya tano?

Kila hoja ijibiwe, kwa elimu na mizani
Na hoja ikaririwe, na dalili ziwe ndani
Nuni na wau zitiwe, na tamko fasilini
Wema umejibu nini, fumbo la wau na mim?

Nae Abul shairi, na nyamaume tokezeni
Tuyatunge mashairi, ya kila nui na fani
Yasomwe kwa kukariri, yalete sifa nchini

Wema umejibu nini, wema na mahali pake?

Sheikh Kaluta Amri Abedi (Simba wa Kwa Lumona) – Dar es salaam

Somo Kutoka Pretoria

Kutoka uk. 5

mateso makubwa yaliyochangia kifo cha Bi. Hadija (ra). Kwa amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alifanya hijra (kuhama) na kuendesha serikali huko Madina. Wenye husda hawakuridhika, wakiwa na wingi wa bughuda mioyoni mwao walifanya hila hadi Mtume wa Mwenyezi Mungu alilazimika kulinda dola la Kiislam na kuimarisha uhuru wa kuabudu. Hakutaka vita asilani. Lakini vita ilipotokea akaonesha jinsi gani binadamu anatakiwa aendeshe mambo wakati wa vita, wazee, watoto hawaguswi. Nyumba za ibada zinalindwa, ni dhahiri Mtume wa Mwenyezi Mungu aliingia vita vya kujihami shingo upande na hiyo ndiyo maana ya kulazimishwa kula nguruwe. Hoja inajengeka ya kuonesha kuwa moyo wake Mtukufu Mtume (saw) ulikuwa baidi na mambo yote yanayohusu vita. Kwani yeye aliletwa kuwa rehema kwa viumbe wote. Lakini hali halisi inatakiwa kuikabili jinsi ilivyo.

Mtu mwingine katika historia ambaye alilazimishwa kutumia mabavu ili kurejesha heshima ya watu wake ni Madiba Mandela. Tutajaribu kuonesha ni hali ipi ambayo ilimnyima kupumua kiasi ya kwamba njia iliyobaki ilikuwa ni utumiaji wa mtutu wa bunduki. Mandela hakuwa gaidi au jambazi, zilikuwepo kanuni zilizotawala mapambano yale. Haikuwa ni kuuwa watu holela. Nia ilikuwa ni kuharibu sekta za uchumi ili wasio na uwezo wa kusikia waweze kusikia. Mipango ya mapambano ilikuwa madhubuti na ililenga shabaha ya kufikisha ujumbe kwamba tunataka uhuru wetu. Kabla ya kufikia huko ufuatao ni mtiririko wa matukio yaliyomfanya Nelson Mandela asiwe na njia nyingine isipokuwa utumiaji wa mabavu kwani ni kweli kama alivyosema Nabii Issa (as) hufa kwa upanga wale wanaoishi kwa upanga.

Kwa makusudi na kwa kutumia hila na mikakati endelevu serikali ya weupe wachache Afrika ya Kusini walihalalisha utawala wao kwa sera chafu ya ubaguzi wa rangi. Hata yule shujaa wa India Mahatma Ghandi aliwahi kushiriki katika mapambano ya kutokomeza ubaguzi wa rangi huko Afrika kusini. Sera ya 'Apartheid' msingi wake ni dharau na matusi kwa wale ambao ardhi ya Afrika ya Kusini walipewa na Mwenyezi Mungu. Sera ya ubaguzi ilisimama kwenye msingi kwamba mtu mweusi ana upungufu wa akili, na hivyo hawezi kushindana na mtu mweupe. Hivyo watu hawa (weusi) lazima watengwe. Hivyo nchi ya Afrika ya kusini likawa ni taifa moja lenye mataifa mawili. Neema zote za nchi kwa weupe na kazi zote za kupiga pasi na ulaji wa makombo kwa watu weusi. Ardhi yote itatwaliwa na weupe. Mishahara ya kichekesho ikatolewa kwa watu weusi, hali ambayo ilimfikisha mwandishi maarufu wa riwaya kutoa kilio 'cry the beloved country'. Mateso haya yaliendelea kwa muda mrefu hadi 1912 wazalendo wa Afrika ya Kusini wakaanzisha umoja wa kudai haki. Umoja ambao ulichukua sifa ya kuwa miongoni mwa vyama vya mwanzoni vya siasa Afrika. Umoja huu uliitwa 'African National Congress'. Chama hiki kilikuwa ni kwa ajili ya watu wote wa Afrika ya Kusini bila kujali rangi zao, makabila yao na dini zao. Kilidhamiria kupigania Demokrasia na uhuru wa kutoa maoni. Kwa njia ya kistaarabu kiliendelea kutetea haki za wanyonge wa Afrika ya Kusini bila utumiaji wa mabavu au fujo za aina yoyote.

Ndoto 3 tukufu za Mtume Muhammad s.a.w

Ustadhi ***A .R. Mikila – Morogoro***

Kutoka toleo lililopita

NDOTO ZA MTUME MUHAMMAD (SAW).

5- Safari ilikuwa ya ghafla, Mtume (saw) hakuwa na taarifa ya safari kabla, wala wakati wa safari hakujua anaenda wapi na kwa madhumuni gani.

- Mtume (saw), hakuweza kuuliza hayo, wala kuhoji jambo lolote. Yeye aliharakia kinyume na desturi yake, akaanza safari bila hata ya kumuaga mkewe kipenzi Bi Khadija. Wala watu wa nyumbani mwake. Kindoto hali hiyo inakubalika, alienda kindoto, akarudi kindoto bila hata wengine kujua wala kumuona au kuhisi kutokuwepo kwake.

6- Kuingia kwake peponi kwa saa chache na kisha kutoka na kurudi duniani.

- dhahiri hayo ni matendo ya kindoto. Ndotoni kila jambo linawezekana, lakini kimwili mengi hayawezekani. Pepo na moto, kiistilahi ni tunzo au malipo maalum ya kiroho. Mtu ameahidiwa kupewa baada ya kufa, ni malipo ya mwili wa kiroho siyo ya mwili huu wa kidunia.

Naamini mpka hapa msomaji wangu, nitakuwa nimekusaidia sana kuifahamu hakika ya Mi'raji na uhalisia wake.

NINI KILITOKEA BAADA YA NDOTO HII?

Hebu sasa tuyatazame yale yaliyojiri baada ya Mtume (saw) kuota ndoto hii.

01- **MILANGO YA UISLAM KWENDA NJE YA MAKKA ILIFUNGUKA.**

Wakati ndoto hii inaotwa na Mtume (saw), hali ya usalama kwa Waislamu pale Makka, ilikuwa ni mbaya. Walikuwa katika wakati mgumu na wa mateso makubwa. Mateso haya yaliyo kithiri, yalimlazimisha Mtume s.a.w, afikirie hatua nzuri ya kuinusuru dini na waumini wake. Hapo akapata wazo la kuwashauri waislamu kwamba, ni heri baadhi yao waihame Makka na kwenda kuishi Uhabeshi (Ethiopia). Nchi ya Uhabeshi ilikuwa ikitawaliwa na mfale Najashi aliyekuwa mkristo. Mfalme huyu alikuwa mtu mwema na muadilifu sana. Mtume s.a.w, aliwataka waislamu wahamie kule ili wakapate hifadhi na maisha ya amani. Bila shaka alilenga kufikisha mafundisho ya Islam upande ule pia. Waislamu kadhaa waliupokea ushauri huu na kuufanyia kazi. Wale waliojipanga kuihama Makka, waliihama na kwenda Ethiopia. Kule wakapokelewa vizuri, wakapewa makazi na kuanza maisha mapya ya amani na utulivu. Ndani ya Uhabeshi waislamu hawa, wakawa ni kikundi maalum cha wachamungu wakimbizi wenye umoja. Hii ndiyo hatua ya kwanza iliyo chukuliwa na Mtume (saw), baada ya Miraji na amri ile ya Sala. Alichukua hatua ya kuanzisha umoja wa namna yake na kuanzisha mshikamano huu. Neno 'Sala' maana yake nyingine ni mshikamano maalum wa watu kiimani na uzalendo.

Mahasimu wa uislamu na wafuasi wao, walituma kikosi maalum cha wajumbe kwenda Ethiopia, kuwafata ndugu hawa ili kuwarudisha Makka kwa nguvu. Walipofika Uhabeshi, walijaribu kwa hila, kutoa maneno ya fitina kwa Mfalme na serikali yake kwamba, mafundisho ya Waislamu wale yana mkashifu Yesu Kristo na mama yake, na kwamba ni vema watu hao wafukuzwe na wakabidhiwe kwao ili warudi nao Makaa. Mfalme Najashi hakushawishika kuwafukuza waislamu wale au kuwakabidhisha kwa mahasimu hao.

Hapa Mfalme Najashi anaonekana kama ndiye kiongozi wa mabawabu aliokutana nao Mtume s.a.w kule mbinguni katika usiku wa Mi'raji. Bila shaka hii ndiyo ile mbingu ya pili, aliyo iona Mtume (saw) imejaa amani na utulivu, iliyo kaliwa na Nabii Isa (as) na Ardhi yake imejaa manukato ya uturi. Katika mbingu hii, mbele ya baraza la Mfalme huyu, Sayidina Jaafari bi Abu Twalib (r.a), Kiongozi wa Waislamu wale wakimbizi, alimsomea Mfalme Najashi Qur'an, sura Mariyam kwa unyenyekevu na utulivu sana:- "Na umtaje Mariyamu kitabuni alipojitenga na jamaa zake akaenda mahali upande wa Mashariki Na akaweka pazia kujikinga nao. Kisha Tukampelekea Malaika Wetu aliye jimithilisha kwake kama mtu kamili….Ewe dada wa Haruni, baba yako hakuwa mtu mbaya wala mama yako hakuwa asherati. Ndipo akashiria kwake (*Issa).* Wakasem:Tutazungumzaje na aliyekuwa mtoto kitandani? (*Issa)* Akasema:Hakika mimi ni Mtumishi wa Allah, Amenipa kitabu na Amenifanya Nabii. Na Amenifanya mbarikiwa popote nilipo. Na Ameniusia Sala na Zaka madamu ningali hai. Na kumfanyia mema mama yangu, wala Hakunifanya niwe jeuri mwenye bahati mbaya. Na amani iko juu yangu siku niliyo zaliwa na siku nitakayo kufa na siku nitakayo fufuliwa hai. Huyo ndiye Isa bin Mriyamu, (hiyo) Ndiyo kauli wanayo ifanyia shaka….."(Kur 19:17-41).

Sayidina Jaafari (ra), alimdhihirishia Mfalme Najashi ni kiasi gani mafundisho ya dini ya Islam yanavyo muheshimu Nabii Isa (as), pamoja na mama



Ustadh Abdulrahman Mikila

yake Mtukufu. Alisema Qur'an inawatambua sana watu hawa kuwa, walikuwa ni watukufu na watawa sana.

Mfalme Najashi aliguswa sana na maneno haya ya Qur'an juu ya nabii Isa na mama yake. Akatangaza kukubaliana na maelezo yale na kupinga shutuma zote za ujumbe ule wa watu wa Makka. Mfalme Najash alisema kwamba, hadhi ya Yesu Kristo mbele yake yeye, haiendi umbali wa hata hatua moja iliyo sawa na kijiti alichoshika mkononi, kutoka pale Qur'an ilipo ishia. Kwa maneno yale ya Mfalme yakijasiri na uchamungu, Amri bin Al'asi, aliye kuwa kiongozi wa ujumbe wa Makafiri wa Makka, alifadhaika sana. Alirudi Makka akiwa mnyonge na huzuni usoni. Bwana huyu baadaye sana alikuja kusilimu.

Kupitia safari hii ya Mi'raji, Afrika ilipata Baraka ya kuwa mfariji na muhifadhi wa kwanza wa Masahaba watukufu wa Mtume (saw). Afrika ililetewa na kusomewa Qur'an ikiwa bado changa. Amani kwa Ethiopia, Amani kwa Bara la Afrika na Amani kwa mfalme Najashi.

02- Mi'raji ilileta mshikamano

Mpango wa safari ya kwenda uhamishoni Uhabeshi, ulikuwa ni wa siri, kama vile ilivyokuwa siri ile safari ya usiku wa Mi'raji. Mpango ule haukutakiwa ufahamike kwa maadui wa waislamu. Kwa hiyo pendekezo lile la kuwataka baadhi yao waihame Makka lilipo tolewa, wahamaji walitakiwa kuandaa mpango maalum wa pamoja na wa siri. Vikao vyao vya maandalizi na namna ya kukutana hadi kuanza safari, havikutakiwa vijulikane.

Sayidina Umar akiwa bado hajasilimu na mwenye uadui dhidi ya uislamu, kwa bahati tu, akawafuma waislamu hawa wakijipanga kuondoka Makka. Alishangaa kuona mizigo imefungwa kisafari. Akawauliza vipi, ndiyo mnaondoka? Mama mmoja, Ummu Abdallah akamjibu ndiyo! Mungu ni shahidi yetu. Tunaenda nchi nyingine, ninyi hapa mnatutesa na kututendea mambo ya ukatili sana. Hatutarudi mpaka Mwenyezi Mungu apende kuturudisha. Maneno haya ya ukakamavu yaliyojaa simamanzi na uchungu, yaliugusa sana moyo ya Sayidina Umari. Hapo aliduwaa akakaa kimya kitambo akitafakari, kisha akasema Mungu awe pamoja nanyi.

Hii ndiyo taathira iliyo letwa na Mi'raji katika moyo wa Sayidina Umari bin Khatwabu. Baada ya miezi michache kupita, Umari bin Khatwabu akasilimu. Masahaba kwa furaha walisema *Allahu Akibaru, Allahu Akibaru*. Kauli hii ya *Allahu Akibaru,* ilitolewa na Nabii Ibrahimu Mbingu ya saba katika usiku ule wa Mi'raji.

03 – Mi'raji ilileta upendo

Lipo tukio moja kubwa la kihistoria linatajwa kutokea mjini Makka, kuhusiana na Aya ya 63 ya Sura Anajim. Inasimuliwa kwamba, miezi michache tu kupita, tangu baadhi ya waislamu kuihama Makka na kwenda Ethiopia; Mtume (saw), siku moja alienda mitaani kuhubiri. Wakati anahubiri katika mtaa fulani, kukawepo na mkusanyiko wa watu wengi. Kwa kudra maalum, akajikuta amesoma sura hii ya An Najim, Alipoifikia Aya ya 63, yenye maneno "Basi msujudieni Allah na kumuabudu", Mtume (saw) alianguka kusujudu.

Kwa namna ya ajabu sana, watu wote waliokuwepo katika hadhara ile, waislamu kwa wapagani na wengineo, wote walianguka kusujudu pamoja naye. Sijida hii adhimu na tukufu, iliwasisimuwa sana wale walioshiriki, kiasi cha kudhaniwa kwamba Maquraishi wote wa Makka wamekwisha silimu. Tukio hili likavumishwa hadi Ethiopia na kuwafanya baadhi ya Muhajirina kurudi Makka kwa haraka na kwa shangwe kubwa la matumaini ya amani na usalama.

04 - Miraji ilifungua Tablighi nje ya Makka

Wale waislamu walio kwenda Ethiopia waliamsha tashwishi za watu juu ya itikadi na imani mpya ya kidini. Waethopia kabla ya ujio wa waislamu, walikuwa wakiijua dini ni upagani na Ukristo, lakini sasa ikaongezeka dini nyingie mpya. Kwao hili, ilikuwa ni jambo jipya na dini mpya ya kujifunza. Mfalme Najashi pamoja na watu wake walijilazimisha kuijua dini hii ya Islamu. Na kwa kiasi kikubwa iliwabadilishia muelekeo wa maisha yao. Mtume s.a.w, alipopata habari ya kifo cha Mfalme huyu alisalisha Sala ya jeneza ghaibu kwa heshima yake.

05 - Miraji ilijenga taswira ya Waumini wa Islam.

Wapagani wa bara Arabu na hata huku Afrika, hawakuwahi kupigana na kudhulumiana kwa sababu ya itikadi za kidini. Kwao wao ilikuwa si lawama kwa mtu au kikundi chochote cha watu kuabudu chochote, liwe Jua, Nyota, Jiwe au au hata Mti. Ethiopia ilishangaa kuona Waarabu wameingia katika tabia ya Warumi na Wayahudi wa kale. Warumi na Wayahudi waliwatesa wakristo kwa sababu ya hitilafu za kiimani.

Jambo hili liliamsha kumbukumbu za mfalme Najashi, juu ya mateso ya zamani aliyo yapata Yesu Kristo na wafuasi wake. Mfalme Najash akapata kuona kwa ukaribu zaidi na kwa uhalisia halisi, hali ya watu wanao kubali mateso na kuyavumilia kwa ajili ya dini.

Fundisho la Qur'an Tukufu lina wataka na kuwahimiza waislamu, waige mfano wa wafuasi wa nabii Isa (as), wa kuwa na subira na kutawakali kwa Allah:-

" Enyi mlioamini kuweni wasaidizi wa Allah, kama alivyo sema Isa bin Mariamu, kuwaambia wanafunzi (wake): Ni nani wasaidizi wangu kwa ajili ya Allah, wanafunzi wakasema sisi ni wasaidizi wa Allah. Basi taifa moja la wana wa Israeli waliamini na taifa linguine wakakufuru;

ndipoTukawasaidia wale walioamini dhidi ya maadui zao, na wakawa ni wenye kushinda"(61: 15).

Kwa hakika Mi'raji ilikuwa ni taswira ya mabadiliko aliyo onyeshwa Mtume (saw), ya kukua kwa dini ya Islam, lakini makafiri hawakujua hili.

06 - Miraji iliwabadilisha mawzo watu wa Makka

Kuhama kwa baadhi ya waislamu na kwenda nchi nyingine, kuliwasitua wakuu wa Makka. Maqureishi kwa ujumla wao, walijihesabu kuwa ndiyo walinzi wakuu wa Kaaba. Tendo la mtu kuihama Makka, lilihesabiwa kuwa ni uhaini. Ndiyo maana hawakuvumilia kuona waislamu wanaihama Makka na kuiacha Kaaba bila ulinzi. Kwao Kaaba ni alama ya utukufu wa Allah na utukufu wao pia. Iweje basi wavumilie kuona watu wake wanaihama Makka na kuiacha Kaaba ukiwa?

Muhamo ule wa baadhi ya waislamu uliwafanya vijana wengi wa Makka na hasa walala hoi wajiulize kulikoni? Kwa sababu hiyo walikuwa wanakusanyika kila aendako Mtume (saw). Hali hii ndiyo iliyo sababisha siku moja wao, wasujudu pamoja na Mtume (saw), pale aliposoma Sura Najim, Aya ya 63 mbele ya mkusanyiko mkubwa wa watu.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

TANGAZO LA IJTMAA YA 25 YA MWAKA 2014.

Kwa Khuddamul Ahmadiyya na Atfalul Ahmadiyya wote Tanzania

Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania inawatangazia wanatanzeem wote kuwa, Ijtmaa ya 25 itafanyika Dar es Salaam kuanzia tarehe 20 hadi 22 mwezi wa 6 katika viunga vya Jumuiya Ahmadiyya Kitonga. Wanatanzeem wote tunaombwa kujiandaa na kushiriki katika tukio hilo muhimu na kushiriki mashindano mbalimbali yatakayofanyika. Watu wote na watakaotoka mikoani wajitahidi kuwa kitonga kabla ya sala ya Ijumaa ya tarehe 20 kwa maandalizi muhimu. Aina ya mashindano yatakayofanyika yanahitaji maandalizi na yatakuwa kama ifuatavyo:

Mbashiri Mkuu Dodoma na Singida

Kutoka uk. 1



Masjid Khurshid - Msikiti wa Ahmadiyya Manyoni, Singida

katika swala zima la ufikishaji wa ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa (as).

Katika kufanikisha hilo Amir na Mbashiri Mkuu aliwataka Wanajumuiyya kuwa wakweli siku zote na muda wote na kuishi kwa kufuata nidhamu ya Jamaat katika muda wote wa maisha yao, tena aliwasisitiza Wanajumuiyya kutorudia makosa ya zamani bali wafuate taratibu na nidhamu hasa ya Jamaat sawa na mafundisho ya Seyyidna Ahmad (as) mwenyewe ikiwa ni pamoja na kujitahidi sawa na uwezo, kusali sala ya Tahajjudi. Katika ziara yake Amir na Mbashiri Mkuu pamoja na mambo mengine pia alifungua rasmi Misikiti ya Kinyeto na Kitumbili (Manyoni) sambamba na ufunguzi huo pia alitoa nasaha kwa Wanajumuiyya pamoja na wageni waalikwa, jambo la kwanza wanalotakiwa kulifanya ni kuwa wanamcha Mwenyezi Mungu kwa vitendo hasa si kwa kukiri tu pia alisisitiza Waaminio kujitolea kuinua Uislam nchini na Duniani kwa ujumla, na aliwataka watu wote kuitumia misikiti hiyo kwa kufanya ibada bila ya hofu yoyote kwani, misikiti ni nyumba ya Mwenyezi Mungu haijalishi imejengwa na nani. Hivyo tufanye ibada bila ya hofu yoyote ile.

Amir sahib na Mbashiri Mkuu alisisitiza kuwa ni maagizo ya Mtume (saw) kutafuta elimu kwa kila hali ili upate kumtambua Mwenyezi Mungu pia alisema katika kufanikisha haya yote amani na utulivu uliopo ni muhimu. Ni lazima jamii iliyopo ijenge tabia ya kuheshimiana mkubwa kwa mdogo na mdogo kwa mkubwa, pia mwenye nacho kwa asiye nacho, aidha alisisitiza tuzingatie mambo yote tunayoagizwa na Mwenyezi Mungu ili tupate radhi yake. Inshallah.

UFUATAO NI MPANGILIO WA MASHINDANO YA IJTIMAA YA KHUDDAM ITAKAYO FANYIKA TAREHE 20-22 JUNE 2014.

AINA YA SHINDANO	KHUDDAM	ATFAL
1. QURAN A) HIFDH	JUZUU YA 30; JUZUU YA 29 NA 30 JUZUU YA 28,29 NA 30; JUZUU YA 26,27,28,29 NA 30	SURA MBALIMBALI JUZUU 30; JUZUU YA 29 NA 30 JUZUU YA 28,29 NA 30 JUZUU YA 26,27,28,29 NA 30.
B) TAFRISI	SURAT AL-FURQAN (25:62-78).	SURAT BAQARA (2:1-17)
C) TILAWAT UL QURAN (USO-MAJI)	MSOMAJI ATAPEWA SEHEMU YEYOTE KUSOMA KWA KU-FUATA KANUNI	MSOMAJI ATAPEWA SEHEMU YEYOTE KUSOMA KWA KUFUATA KANUNI
2) HADITH	HADITH ZA MTUME (s.a.w) KUTOKA KITABU CHA KI-UNGA CHA WATU WEMA KUHUSU SALA (KUANZIA NO 187-196)	(A) {i} HADITH AROBAIN PAMOJA NA MAELEZO YAKE, HADITH NO 1-20. {ii} KIUNGA CHA WATU WEMA, HADITH NO. 25 NA 28. (ATFAL WA MIAKA 11-15)
		(B) HADITH AROBAINI BILA YA MAELEZO (ATFAL CHINI YA MIAKA 10)
3) HOTUBA	"HISTORIA YA TANZEEM YA KHUDDAMUL AHMADIYYA TANZANIA NA UMUHIMU WA VIJANA KATIKA KUHUDUMIA ISLAM".	ATFAL ACHAGUE KICHWA KIMOJA TU KATI YA VINGINE NA AANDAE HOTUBA YAKE. (i) UPENDO WA MTUME KWA WATOTO (ii) FAIDA ZA SALA YA KIISLAM (iii)KUTANGULIZA DINI JUU YA DUNIA
4) SHAIRI	KUTUNGA SHAIRI PAMO-JA NA KUGHANI. SHAIRI LIWE LIMEBEBA UJUMBE UFUATAO. "MAAJABU YA KITABU CHA MANANI, QURANI"	KUGHANI SHAIRI LENYE UJUMBE WA "MIAKA 75 YA TANZEEM YA KHUDDAMUL AHMADIYYA"
5) SALA YA KIIS-LAM	FARADH ZA MAITI KWA VI-TENDO. (KWA MWANAUME) -KUOSHA -KUVESHA SANDA -SALA YA JENEZA -KUZIKA	(A) KUONYESHA MFULULIZO MZIMA WA SALA KWA VITENDO (ATFAL CHINI YA MIAKA 10)
		(B) {i} SALA YA JENEZA KWA MWANAUME, MWANAMKE NA MTOTO MDOGO. {ii} DUA YA KUNUTI-SALA YA WITRI. {iii} HOTUBA YA PILI YA IJUMAA-(ATFAL WA MIAKA 10-15)
6) MAOMBI.	(i) KUTOKA KITABU CHA MAOMBI YA MTUME (S.W.A) NO 65-74 (ii) KUTOKA MAOMBI YA QURA-NI TUKUFU KUANZIA No 02- 07.	KUTOKA KITABU CHA MAOMBI YA MTUME (S.A.W) DUA NO 1-20
7) QUIZ	WATAULIZWA MASWALI MBALIMBALI.	WATAULIZWA MASWALI MBALIMBALI.

MICHEZO:

Khuddam

(1) Kuvuta kamba (2) Mpira wa miguu (3) Riadha
(4) Mieleka ya mezani kwa mikono. (5) Volleyball
(6) Kuandika taarifa ya tukio ulililoliona

Atfal

(1) Kuvuta kamba (2) Kukimbia kwa magunia
(3) Mpira wa miguu (4) Riadha. (5) Mashindanoyaziada.

Majlis Khuddamul Ahmadiyya inawatakia maandalizi mema kwa kumtaka kila Khuddamul Ahmadiyya na Atfalul Ahmadiyya Tanzania ajipange kuhudhuria na kushiriki kwenye Ijtmaa hiyo.

ZINGATIA:

- KILA KHUDDAM NA ATFAL ANATAKIWA KUHUDHURIA IJTIMAA HII INSHA-ALLAH
- KWA MATAWI YA MKOA WA DAR ES SALAAM KILA TAWI LITOE WASHIRIKI WATATU KWA KILA SHINDANO.
- PWANI, MIKOA YA KUSINI NA MOROGORO-KILA MKOA WAPATIKANE WASHINDI WATATU (3) WATAKAO SHIRIKI KILA SHINDANO LA IJTIMAA.
- MATAWI YALIYOBAKI-ANGALAU KILA TAWI LITOE MSHIRIKI MMOJA KWA KILA SHINDANO.

Imetolewa na ofisi ya:

SADR MAJLIS KHUDDAMUL AHMADIYYA TANZANIA
Dr. SWALEH KITABU PAZI-
Mob: +255 713995804. Email-tzkhuddam@yahoo.com

Waislam zingatieni Onyo la Allah

Na Omari Sebuge;
Mpanda – Rukwa

Mwenyezi Mungu Anasema;
"Wala msiwe kama wale waliofarikiana na kuhitilafiana baada ya kuwafikia dalili zilizo wazi na hao ndio watakaokuwa na adhabu kubwa" (Qur'an Tukufu 3:106).

Hili ndilo onyo la Mwenyezi Mungu kwa Waislamu kwamba wasije wakafarikiana na kugawanyika kama vile Mayahudi na Manaswara walivyogawanyika makundi makundi. Akisisitiza juu ya kushikamana Anasema;
"Na shikeni kamba ya Allah nyote, wala msiachane, na kumbukeni neema ya Allah iliyo juu yenu mlipokuwa maadui naye Akaziunganisha nyoyo zenu, hivyo kwa neema yake mkawa ndugu, na mlikuwa ukingoni mwa shimo la moto naye Akawaokoeni nalo. Hivyo ndivyo Allah Anavyokubainishieni aya zake ili mpate kuongoka". (Qur'an 3:104).

Mwenyezi Mungu Anapoonya juu ya jambo fulani anajua litafanyika tu, hivyo Anaonya mapema ili likitokea wasije wakasema hawakuonywa kwalo. Mbali ya kuonywa, Mwenyezi Mungu Anawabainishia Waislam kwamba na wao watafarakana na kugawanyika. Anasema; "Na kama Mola wako Angalipenda bila shaka Angaliwafanya watu kuwa ummati mmoja. Nao wataendelea kuhitilafiana" (11:119)

Anasema; Anao uwezo wa kuwafanya watu wawe kundi moja bila ya kuhitilafiana kama malaika walivyo, lakini watu wamepewa hiyari ya kuchagua kutii amri za Mwenyezi Mungu au kutozitii, kwa hiyo maadamu shetani anaendelea kuwepo na waovu bado wapo, ni sharti mifarakano na migawanyiko itokee kwa Waislam pia. Kufarikiana na kuhitilafiana katika dini ni jambo linalomchukiza sana Mwenyezi Mungu, tukisoma Qur'an Tukufu 10:20 Allah Anasema; "Wala watu hawakuwa ila kundi moja, lakini wakahitilafiana. Na kama si neno lililotangulia kutoka kwa Mola wako, bila shaka shauri lingekwisha katwa baina yao katika yale waliyohitilafiana". Pia Anasema;
"Na hawakutengana ila baada ya kuwafikia elimu, kwa sababu ya uasi baina yao, na kama isingalikuwa kauli iliyotangulia kutoka kwa Mola wako juu ya muda uliowekwa, hukumu ingalitolewa baina yao …." (Qur'an Tukufu 42:15).

Aya hizi na nyingine huonyesha jinsi gani Mwenyezi Mungu Anavyowachukia watu wenye kufarakana na kuhitilafiana juu ya dini yake, anasema; Laiti siku ya kiyama isingewekekewa muda maalum, bila shaka wangalikwisha kuhukumiwa zamani. Mwenyezi Mungu Ameweka utaratibu kwamba pindi watu wanapofarakana na kuhitilafiana kiasi cha kugawanyika makundi makundi, huwaletea mwonyaji mwenye kuwasuluhisha na kutoa hukumu kwa uadilifu juu ya hitilafu zilizoingizwa katika dini, wenye kumkubali na kumfuata huungana tena na kuwa kundi moja, itikadi moja chini ya kiongozi mmoja.

Hasira ya Mwenyezi Mungu juu ya kufarikiana na kuhitilafiana katika dini, inadhihirika zaidi pale Alipomwagiza Mtume wake (saw) maneno haya;
"Hakika wale waliofarikisha dini yao na wakawa makundi makundi huna uhusiano nao wowote. Bila shaka shauri lao ni kwa Mwenyezi Mungu kisha atawaambia yale waliyokuwa wakitenda". (Qur'an Tukufu 6:160)

Kwa mujibu wa aya hii, watu wanapohitilafiana katika dini na kugawanyika makundi makundi huhesabiwa wenye kukata uhusiano baina yao na Mtume wao, na kukata uhusiano na Mtume ndiyo kukata uhusiano na Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo Mwenyezi Mungu Alipowaonya Waislam wasifarikiane na kuhitilafiana kama wenzaowaliowatangulia, maana yake ni hiyo hiyo ya kwamba na wao wakifanya hivyo watakuwa wamevunja uhusiano baina yao na Mtume (saw).

Mtume (saw) alipowatangazia masahaba juu ya Waislam wa zama za mwisho watakavyogawanyika na kushika mwenendo wa Mayahudi na Manaswara shubiri kwa shubiri, masahaba walifadhaika sana kuhusu uhai wa Uislam. Bali Mtume (saw) aliwapa moyo alipowaambia kuwa; maadamu yeye yupo mwanzoni na Masihi kuwepo mwishoni, Uuislamu kamwe hauwezi kuangamia.

Waislam wakatambua kwamba, watakapofarakana na kugawanyika Mwenyezi Mungu Atamleta Masihi ili awe mwonyaji na hakimu muadilifu, atakayehukumu juu ya hitilafu zitakazoingizwa katika Uislam, na kuwarudisha Waislam katika umoja wao wakiwa na itikadi moja chini ya kiongozi mmoja.

Utabiri wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake (saw) kuhusu Waislam kuhitilafiana na kugawanyika, umetimia, lakini bahati mbaya sana ibilisi amefanikiwa kuwadhanisha Waislam wote wa zama hizi za upotevu kwamba Masihi aliyetabiriwa ni Isa mwana wa Mariamu wa Uyahudi, ambaye aya kadhaa za Qur'an na Hadithi za Mtume (saw) huthibitisha waziwazi kuwa Isa mwana wa Mariam amekufa kifo cha kawaida naye hawezi kurudi tena hadi siku ya ufufuo. Hivyo Mwenyezi Mungu Alipomtuma Masihi, mfano wa mwana wa Mariamu (Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad as) mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya, wakamkataa na kumdhihaki, hadi sasa wanaendelea kumsubiri Nabii aliyekwisha fariki awashukie kutoka mbinguni.

Tunawaomba sana jamaa zetu Waislam watambuwe kuwa kwa mujibu wa aya niliyoinukuu hapo juu, maadamu mmehitilafiana na kugawanyika vikundi vikundi vyenye kufarakana kiasi cha kuuwana wenyewe kwa wenyewe, tayari mmekwishavunja uhusiano baina yenu na Mtume (saw) na Mtume (saw), tunawapa habari njema wale wote wenye mioyo safi kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake (saw) imeshatimia zaidi ya miaka mia moja iliyopita, Masihi na Imamu Mahdi aliye hakimu mwadilifu keshafika naye siye ila ni Mirza Ghulam Ahmad (as) wa Qadian, wahini mje kumpokea na kumfuata kwani Mtume (saw) ameagiza kuwa; atakapofika Masihi ni juu ya kila mtu kumfuata na kumkubali japo alazimike kutambaa juu ya barafu hadi afike aliko. Yaani kumfuata ni jambo la lazima hata kama mtu alazimike kukabiliana na taabu ya aina yoyote.

Ama wale wenye mioyo migumu wasiopenda kusikia wala kuona, hatuna cha kuwaambia, ila maneno haya ya Mwenyezi Mungu;

"Na mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na jihadharini. Lakini mkikengeuka, basi jueni ya kwamba juu ya Mtume wetu ni kufikisha tu (ujumbe) waziwazi". (Qur'an Tukufu 5:93). Kisha Anasema;

"Na sema; Ukweli umetoka kwa Mola wenu, basi anayependa akubali na anayependa basi akatae. (Lakini watakaokataa) hakika tumewaandalia wadhalimu moto ambao ua wake utawazunguka. Na wakiomba msaada, watasaidiwa kwa maji kama shaba iliyoyeyuka yatakayoziunguza nyuso. Kinywaji kibaya kilioje, na mahali pabaya palioje, pa kupumzikia". (Qur'an Tukufu 18:30)

Haya ya Ikwiriri Umeyasikia?

Nusura wauwane. Alama ya Kibla, uzio wa wanawake, Mnara wa msikiti vyavunjwa. Vya daiwa ni ishara ya shetani, waumini wagawanyika.

Na Mwalimu Nassoro Hussein – Kibiti, Pwani.

Takriban miaka miwili hivi imepita tangu pale vuguvugu la Mawahabi (Wahabiya) lilipoanza katika mji wa Ikwiriri. Hawa mabwana walipoingia katika mji huu walikuja na sera ya 'Nusra', yaani wakiwa na maana ya mpango maalum wa kuihami dini chambilecho Jihadi.

Waliendelea kuhamasisha kupitia sera zao hizo na polepole walianza kupata wafuasi hususan vijana, akina mama na hata wasichana. Kutokana na wingi huo wa ghafla, ikaonekana sasa ni muda muafaka wa kujenga msikiti kwa ajili ya kufanyia ibada. Lakini kwa bahati mbaya, ndugu hawa kama ilivyo kwa Waislam wengine, wa kawaida hawana kiongozi mmoja ambaye anaweza kuwasimamia au kutoa ushauri kama tulivyo sisi Waislam wa Ahmadiyya ambao tunae Khalifa kati yetu. Kwa hali hiyo hata walipoazimia kujenga msikiti huo walijikuta wakikwama, kwa sababu hawakuwa na mtu wa kuwaongoza juu ya jambo hilo.

Kwa hiyo walipokuwa ndani ya duara la mkwamo, wakafanya shura (mashauriano) kama ilivyo maarufu kwao. Sasa kupitia shura hiyo, ikaonekana dhahiri shahiri ya kwamba msikiti hauwezi kujengeka, kwa kuwa nguvu ya ujenzi hawana, na msimamizi pia hawana. Wengine miongoni mwao wakaja na wazo la kumpata mdhamini ambaye atakuwa na jukumu la kuujenga msikiti huo mwanzo hadi mwisho kwa gharama zake mwenyewe.

Kwa kweli wazo hili lilipokelewa kwa shangwe kubwa sana ingawa kwa kufanya hivyo wakasahau ya kwamba walikuwa wanatengeneza sifa ya kuomba omba ambayo ni kinyume cha mafundisho ya Uislam. Kwa hiyo ikaundwa kamati maalum kwa ajili ya kuwatafuta mabwana wenye mapesa, kwa ajili ya kujengewa kile kilichoitwa ni n yumba ya Allah.

Kwa bahati mdhamini alipatikana na walipomuelezea makusudio yao, yule tajiri aliwakubalia kwa masharti haya yafuatayo:-
a) Msikiti ukijengwa yeye ndiye ateuwe uongozi kama vile Imam, Makatibu n.k.
b) Taratibu zote za ibada ziendeshwe kwa mujibu wa madhehebu yake na si vinginevyo
c) Mambo yote kuhusu msikiti na Waumini kwa jumla ni lazima mambo hayo yaripotiwe kwake, akiwa ndiye mdhamini wa Msikiti huo.
Siku zote mtu aombae huwa hana masharti. Hatimae hawa jamaa waliyakubali hayo masharti, kiwanja kikatafutwa na ujenzi ukaanza mara moja tena kwa spidi kali zilizochanganywa na mbwembwe dhidi ya watu wengine wasio kuwa wa madhehebu yao.

Hatimaye msikiti ulikamilika, madrasa ikajengwa, ibada ikawa moto moto, akinababa kwa akina mama, vijana kwa wasichana, ili muradi kila mmoja wao alishiriki kwenye ibada m aana msikiti walioutaka umepatikana. Huku wakiendelea kwenye hali hiyo mashehe kutoka sehemu mbalimbali kwa nyakati tofauti walikuwa wakipewa nafasi ya kutoa mawaidha kwenye msikiti huo.

Katika wahubiri hao wapo waliohubiri kwamba, kwa Mwislamu kusoma shule hizi za kawaida ni ukafiri, hivyo hivyo kwenda hospitali kwa ajili ya matibabu, kwenda kupeleka mashtaka polisi huo ni ukafiri uliopitiliza. Lakini kubwa kuliko yote, ni pale shehe Fulani kutoka Unguja alipouelekea msikiti huo na kusema kwamba hii minara, alama za kibla, huu uzio unaotenganisha akina m ama na akina baba akasema ya kwamba haya yote ni ukafiri mtupu na inafaa vivunjwe kwani ni alama za mashetani havitakiwi kuwepo msikitini.

Waumini nao baadhi yao bila kuuliza wakahamasika, kwa kweli wakavunja mnara, wakavunja alama ya kibla, wakavunja uzio wa akina mama. Lo! Kumbe walikuwa wamesahau yale masharti ya yule bwana mapesa, waliyokuwa wamekubaliana hata msikiti huo ukajengwa, yule bwana alipopata habari kuwa sehemu Fulani za msikiti wake zimevunjwa alichokifanya ni kuifukuza kamati yote ya msikiti, na kisha kuchagua kamati nyingine.

Miongoni mwa wale waliokuwa hawajakubaliana juu ya ubomoaji ule. Na wale waliobomoa wakatakiwa wajenge tena upya minara, kibla na uzio kwa ajili ya kina mama. Lakini kama ijulikanavyo Wahabiya ni wenye kiburi, kwa hiyo walijaribu kutotii amri hiyo. Bosi wao akaenda kuleta polisi, na kwa hivyo wakatii amri hiyo halali, chini ya ulinzi maalum wa polisi. Hapo uadui wa wao kwa wao ukapamba moto waliosema minara ni halali wakabaki na msikiti wao, waliosema minara ni ngujzo ya shetani, wakaondoka wakaenda kujenga nyumba ya mabanzi ya mbao sawa na itikadi zao.

Kwa kupitia makala hii ninawaalika ndugu zangu Wahabiya wote na Waislam wote kwa jumla, njooni mumpokee Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) ili aweze kuwapumzisha kwa kuwatua mizigo mizito mliyonayo hivi sasa. Acheni vurugu za kitoto zinazo wapeleka nje ya njia ya Mwenyezi Mungu.

Mwalimu Nyerere na Waahmadiyya

Kutoka uk. 12

wa dini mbalimbali na wasio na dini kuhudhuria kipindi chake.

Sheikh Mubarak Ahmad aliendelea kueleza ya kuwa Islam pekee ndiyo dini iliyokuwa imeletwa kwa binadamu wote na akasema ya kwamba binadamu wote kwa njia moja ama nyingine wamepata manabii. Na kwa sababu ya ukosekanaji wa mawasiliano manabii walikuwa ni kwa makabila na kwa mataifa na akasisitiza ya kwamba mtukufu Mtume Muhammad (saw) ndiye Mtume pekee aliyedai kukusanya mafundisho ya mitume wote waliopita. Akatoa mfano ya kwamba Biblia inakataza kabisa kula nyama ya nguruwe, Sheikh Mubarak Ahmad alipotoka darasani huko nyuma aliacha tufani ya mijadala na wengi walibishana kwa jazba za kukaribia kukunjana mashati.

Vijana wa Kikristo walisema ya kwamba sisi tunajua fika kwamba Waislam hawana elimu. Na wakasema ya kwamba hayo yote aliyoyasema huyo Sheikh wa Waislam ni uzushi mtupu. Hivyo wakasema ya kwamba wawasiliane nae na kabla hajaja aje na ushahidi sio wa maneno bali ushahidi wa Biblia. Hivyo wanafunzi walimsubiri kwa hamu na nia yao ilikuwa ni kumuaibisha, kwani walifahamu fika kwamba ushahidi wa namna hiyo haumo katika Biblia.

Alipokuja tena pale shuleni alielezwa kinaga ubaga ya yote yaliyokuwa yametokea kutokana na kauli yake kwamba Biblia imekataza ulaji wa nguruwe. Na hivyo vijana walikuwa wanataka ushahidi. Ni kweli siku hiyo darasa lilifurika. Na wote walikuwa wana hamu ya kusikia jibu la Sheikh Mubarak Ahmad. Kwa hekima na kwa maarifa aliweza kutoa maelezo na taratibu akawaonesha mahala ambapo linapatikana fundisho hilo katika Biblia. Sheikh Mubarak Ahmad aliwaambia wasomi hawatakiwi kujadili mambo kwa jazba, lazima wajenge hoja kwa busara na hekima. Kinachotakiwa katika mjadala wowote sio kupandisha mori bali ni kutoa ushahidi. Alipomaliza hotuba yake hiyo fupi alichukua Biblia na akamuomba mmoja wa vijana aje asome aya hiyo katika Biblia.

Vijana wote katika darasa hilo walikuwa ni kama watu walionyeshewa mvua. Na kwa hakika tukio hili lilimuathiri sana Julius Kambarage Nyerere. Yeye aliwakusanya baadhi ya wanafunzi na kuwaambia ya kwamba hivi leo tumeaibika sana. Ingawaje Biblia ni



Sheikh Mubarak Ahmad (katikati) akiwa pamoja na Sheikh Amri Abedi kushotoni kwake pamoja na wabashiri wengine wa Ahmadiyya.

mali yetu, lakini inaonesha hatuisomi. Na ni kutoka wakati huo akawa msomaji mzuri wa Biblia jambo ambalo hakuwa nalo kabla ya hapo. Ni kweli ya kwamba katika dhehebu la Katoliki baadhi ya vitabu havilazimishwi sana kwa watu kuvisoma. Jambo kubwa alilojifunza katika kadhia hii ni msomi kutotawaliwa na jaziba. Jambo hili aliliona ni la msingi na linaweza kuwa rahisi kama mtu anajenga utamaduni wa kupenda kusoma.

Nijambolakufurahishakwamba wanahistoria wanatakiwa wakati huo hamu na jazba ya kusoma ikaongezeka maradufu. Inasemekana ya kwamba ilikuwa ni muhali kumkuta Julius Kambarage Nyerere bila kitabu mkononi. Na kama hasomi kitabu basi utamkuta anasoma gazeti. Hii ni khulka na tabia ambayo mwandishi wa habari Jenerali Ulimwengu alipomuona Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika uwanja mmoja wa kimataifa akijaza chemshabongo katika gazeti moja la Kingereza. Ni kweli kutoka wakati ule toka alipoambiwa habari ya

wafahamu kwamba tukio hili lilifanikiwa katika kumjenga vizuri kisiasa Mwalimu Julius Nyerere. Ni mambo mawili ambayo aliweza kuyapata katika tukio hili; kwanza ni kuendeleza utamaduni wa kusoma na kujitahidi kujenga hoja. Miaka mingi baadae Julius Kambarage Nyerere wakati huo ameshakuwa Rais wa Tanzania aliwaambia mabalozi wa Tanzania nchi za nje kwamba si vizuri hata kidogo kwa wana Diplomasia kupayuka bali wanatakiwa wajenge hoja.

Nani anayeweza kusema ya kwamba Nyerere hakuwa na uwezo wa kujenga hoja? Ni dhahiri unaweza kutofautiana naye lakini katu huwezi kupuuza hoja zake. Unaweza kutofautiana naye lakini huwezi kupuuza hoja zake. Moja ya mambo maarufu yaliyomletea Nyerere sifa ni uwezo wake wa kujenga hoja. Na akiwa kijana mbichi hoja hiyo ilipandwa ndani mwake na Mwalimu wake Sheikh Mubarak Ahmad. Ni kweli waswahili wanavyosema 'Samaki mkunje angali mbichi'. Mkunjo wa Sheikh Mubarak Ahmad ulimsaidia sana Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika maisha yake ya kisiasa.

Jambo la kwamba kumbe nguruwe amekatazwa katika Biblia lilimsumbua sana Julius. Kumbe alikuwa si msomaji mzuri. Kumbe mambo mengi yalikuwa ni ya kusikia tu. Toka

nguruwe alianza kuisoma sana Biblia. Na bila shaka wale ambao wamewahi kusikiliza hotuba za Mwalimu Nyerere wataona jinsi gani alivyokuwa akinukuu mistari mingi ya Biblia. Na ushahidi mwingine ni ule alioutoa yeye mwenyewe aliposema ya kwamba 'mimi ninatembea na vitabu viwili na daima napenda kuvisoma na kuvirudia mara kwa mara na vitabu hivyo ni Azimio la Arusha na Agano jipya'. Na ushahidi mwingine ni kwamba kutokana na usomaji wake wa kuzingatia ameweza kutunga utenzi ambao unahusu matendo ya mitume ambayo ni sehemu ya Agano jipya. Hili linatukumbusha utenzi wa Injili ulioandikwa na Mathias Mnyampala na kujibiwa na Mwalimu Khamis Wamwera.

Sifa kubwa ya Julius Kambarage Nyerere ukimlinganisha na viongozi wengine wa Afrika ni mapenzi yake ya kupenda kusoma. Profesa Alli Mazrui ametubainishia wasomi wawili na wanafalsafa wa Afrika na akawataja hao kuwa Leopord Sedar Sengho wa Senegal na Julius Kambarage Nyerere wa Tanzania. Kiongozi huyu Julius Kambarage Nyerere wakati wake wa mapumziko anatafsiri michezo ya William Shakespear, *Julius Kaisari na Mabepari wa Venis*. Bila shaka mapenzi yake yana mzizi mrefu na ukichimba sana utakuta ya kuwa kwa kiwango kikubwa mzizi huo umerutubishwa na maji aliyompa Sheikh Mubarak Ahmad. Licha ya usomaji wa vitabu pia alijitokeza kuwa mtunzi mzuri wa mashairi, jambo ambalo hapo baadae tutaliona ya kwamba nalo aliweza kulipata kutoka kwa Ahmadiyya mwingine Sheikh Kaluta Amri Abedi.

Mara ya pili ya Sheikh Mubarak Ahmad kukutana na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ni wakati Sheikh Mubarak Ahmad alipokuwa akienda Mwanza katika safari zake za mahubiri. Na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa njiani kwenda likizo katika kijiji chake Butiama. Katika safari hiyo Sheikh Mubarak Ahmad alinieleza ya kwamba alimweleza kwa kituo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere falsafa ya mafundisho ya Islam. Alimueleza mambo kama jihad ya upanga kuwalazimisha watu kuingia katika Islam ni mafundisho yaliyokuwa kinyume kabisa na dini tukufu ya Islam. Alimueleza pia ya kwamba mafundisho na desturi za kuwa na wake wengi ni jambo ambalo linajitokeza pia katika Biblia, lakini ni Qur'an Tukufu ambayo imeweka kiwango na masharti kadhaa ya kufuatwa. Alimueleza pia juu ya usawa wa binadamu na uhuru binadamu aliopewa wa kushukuru ama kukataa, lakini pia kuwa na uhuru wa kujitawala yeye mwenyewe. Sheikh Mubarak Ahmad anasema ya kwamba katika wakati wote huo, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa kimya akisikiliza kwa makini sana. Na bila shaka hiyo ilikuwa ni alama ya kuelewa yale yaliyokuwa yanasemwa.

Upo ushahidi mwingine ya kwamba Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliweza kuelewa vizuri mafundisho yaliyokuwa yanabainishwa na Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya na kilipotokea kipindi cha kutaka Misikiti yote iwe chini ya baraza la Misikiti, wenye dhamira hiyo wakawa wanataka kuchukua hata msikiti wa Ahmadiyya. Kesi hiyo ilikwenda mpaka kwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na kwa sababu ya kuielewa vizuri Jumuiya ya Ahmadiyya na tofauti yake na Waislam wengine, alitoa uamuzi ambao ulionesha uelewa wake mzuri wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya. Yeye alisema ya kwamba nyinyi mnaotaka kuchukua misikiti ya Ahmadiyya, sharti la kwanza mtangaze kwamba hawa ni Waislam hapo bila shaka mtaweza kuchukua misikiti yao. Huo ulikuwa ni mwiba mkubwa na hivyo dhamira yao ya kutaka kuchukua misikiti ya Ahmadiyya ikawa imegonga m wamba. Miaka mingi baada ya kustaafu kuwa Rais wa Tanzania, alipokuwa anaeleza nyufa zilizomo katika Taifa letu alieleza matatizo yanayotokana na dini. Akasema ya kwamba zipo nchi za Kiislam zinazowatenga na kuwabagua watu ambao hawakubaliani nao na watu hao katika nchi yetu hii wanaitwa Makadiani, lakini wao hawapendi katu kuitwa jina hilo bali wao wanapenda kuitwa Waahmadiyya.

Zilikuwepo pia jitihada za kutunyang'anya kiwanja chetu huko Morogoro ili kichukuliwe na chama cha TANU lakini kesi hiyo ilipofika kwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye alikuwa akiifahamu vizuri Jumuiya hii alisema ya kwamba hapana – hawa ni watu wa dini, waacheni waendelee na shughuli zao za kidini.

Miaka mingi baadae kilipoanzishwa chama cha TANU Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwaendea Waahmadiyya ili watoe msaada wa uchapishaji wa barua za chama. Ni dhahiri katika miaka hiyo ya 50 hapakuwepo na Ofisi yoyote ya maana na mashine za kuchapa isipokuwa makao makuu ya Ahmadiyya msikiti wa Masjid Salaam. Mwalimu Kiziyala ambaye aliwahi kuwa mwanafunzi katika huo msikiti wa Masjid Salaam, alinieleza ya kwamba mara kwa mara alikuwa akimuona Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akija hapa Masjid salaam kwa kazi za kuchapisha barua na anasema baadhi ya viti kwenye mikutano ya chama vilikuwa vinatoka hapa Masjid Salaam. Ni Sheikh Mubaraka Ahmad pia alipohamia Nairobi aliyewaambia waendelee kukisaidia chama cha TANU hapa Dar es salaam na wasaidizi wakubwa hao waliosaidia chama cha TANU kwa hali na mali ni pamoja na Sheikh Abdulkarim Sharma, Sheikh Kaluta Amri Abedi na Jumanne Abdallah.

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliendelea na ushirikiano mkubwa na Sheikh Mubarak Ahmad kwa njia ya kuandikiana na kuonana. Mwaka 1958 Sheikh Mubarak alipokwenda likizo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na viongozi kadhaa wa chama cha TANU walikuja Masjid Salaam katika sherehe za kumuaga. Wote kwa pamoja walikuwa wakimuaga baba yao ambaye alikuwa amewasomesha Tabora, lakini ambaye alikuwa amesaidia sana kwa njia ya maombi na kwa njia ya dhahiri katika kukisaidia chama cha TANU kiende mbele katika mapambano yake dhidi ya Ukoloni wa Kiingereza.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Wasifu wa Maulana Sheikh Abdulkarim Sharma

Kutoka uk. 12

Marehemu Sheikh Sharma sahib alianza masomo yake ya msingi hapo hapo Qadian, baada ya kumaliza shule ya msingi na kupata cheti cha Moulvi Faadhil akaanza masomo yake ya dini ndani ya chuo cha wabashiri, wakati huo akabahatika pia kufanya kazi katika Ofisi ya gazeti la Alfadhal. Mwaka 1939 wakati wa Jubilii ya Ukhalifa, Hadhrat Mulih Mauud Khalifatul Masihi wa pili akamchagua Sheikh Sharma sahib kuwa miongoni mwa vijana walioilinda bendera ya Jamaat Ahmadiyya ilipokuwa inapeperushwa kwenye uwanja wa mkutano, akiwa na umri wa miaka 29.

Marehemu Sheikh Sharma alifanya wakfu na kujitolea maisha yake kuitumikia dini ya Kiislam chini ya utaratibu wa Jamaat Ahmadiyya. Kwa muda wa miaka mitatu mine alijiunga na kulitumikia jeshi la Kiingereza. Kisha mara tu baada ya vita kuu ya pili kwa maagizo ya Hadhrat Muslih Mauud (ra) akaja Qadian mara moja na akaanza kufanya maandalizi ya safari ya kwenda Afrika. Januari mwaka 1948 akaungana na msafara wa Wabashiri watano na kuelekea Afrika Mashariki kwa ajili ya kazi ya kuitumikia Jamaat. Huko afrika Mashariki akaitumikia Jamaat kwa ujumla m iaka 29. Mwaka 1961 nchi za Afrika Mashariki zikagawanyika Kijamaat katika nchi tatu. Tanganyika, Kenya na Uganda, hapo marehemu Sheikh Sharma sahib akateuliwa kuwa Amir na Mbashiri Mkuu nchini Uganda. Hivyo hivyo yeye alipata pia fursa ya kuitumikia nchi ya Kenya akiwa Mbashiri Mkuu na Amir wake. Vilevile aliwahi kufanya kazi katika hadhi ya Amir na Mbashiri Mkuu nchini Tanzania.

Kuanzia mwaka 1978 akawa anaishi Uingereza, katika kipindi cha miaka kumi alifanya kazi ya uongozi wa Majlis Amila akiwa katibu wa Tarbiyyat na pia Katibu wa Rishta nata (Katibu wa mipango ya kuunganisha watu kwa njia ya ndoa). Wakati wa maadhimisho ya sherehe ya Jubilii ya karne ya Jamaat ya Ahmadiyya duniani yeye alikuwa ni mjumbe wa kamati ya maandalizi ya sherehe hizo, hapa Uingereza alikuwa pia mjumbe wa Majlis ya uchaguzi wa Ukhalifa yeye katika maandiko yake Fulani anaandika tukio moja linaloonyesha ikhlasi ya baba yake, heshima na adabu kwa baba yake pia inadhihirika. Anasema kuwa, mimi nilikuwa nasoma madrasa Ahmadiyya nikiwa katika darasa la nne au la tano hivi, kutokana na sababu fulani moyo wangu ukawa mzito kuendelea na masomo katika madrasa hiyo, nikataka niache jamia nikasome shule ya kizungu katika siku hizo hizo wanafunzi wenzangu wawili wa darasa hilo watoto wa Mzee Hadhrat Maulana Muhammad Ibrahim Bagapuri walikuwa wanasomea huko baada ya kuiacha madrasa ya Ahmadiyya, hivyo basin a mimi nikapata shauku ya kwenda huko.

Mimi mara mbili mara tatu hivi nikaonyesha shauku yangu kwa baba lakini baba hakulishughulikia wazo langu hili. Siku moja tulikuwa tumekaa sebuleni karibu na jiko asubuhi mimi nikamsisitiza sana baba juu ya suala hilo na nikasema kuwa ndugu zangu wengine umewapeleka katika shule za juu high school kwa ajili ya masomo, kwa nini unanisomesha mimi shule ya madrasa Ahmadiyya ya dini? Baba akajibu kuwa hebu fikiria kuwa mimi nimejiunga na Uislam kutokea Uhindu na ilikuwa ni fadhili ya Allah aliyenijaalia kupata neema ya Islam, lakini mimi ninasikitika sana kuwa sijawahi kuitumikia dini ya Kiislam kwa chochote kile, mimi nina hamu sana moyoni mwangu kuwa mwanangu mmoja aitumikie dini ya Kiislam, ni nia hii ndiyo iliyonifanya nikupeleke madrasa ya Ahmadiyya ukasomee dini ili uwe na uwezo wa kuitumikia dini ya Uislam, lakini wewe unasema kuwa hutaki kusomea dini katika madrasa ya Ahmadiyya. Alipomaliza kusema hivi akainuka akaenda chumbani na kwa hali ya huzuni akasimama na kuanza kusali, marehemu anasema kuwa kwa jazba ya kauli aliyoitoa baba yake na kwa hali aliyokuwa nayo wakati ule vikauathiri sana moyo wangu, usiku sikupata usingizi nikawa namuombea sana dua baba yangu, asubuhi palipokucha mimi nikaahidi kuwa sawa na matakwa ya baba yangu mimi nitaendelea na masomo yangu katika madrasa ya Ahmadiyya.

Hivyo basi, Hadhrat Muslih Mauud alipotangaza vijana wajitolee maisha yao kuitumikia dini mimi nikamwandikia barua Khalifatul Masihi ya kumuomba anikubalie waqfu wangu. Hivyo ndivyo alivyotimiza matakwa ya baba yake na jaziba ikawa imezalika moyoni ya kuitumikia dini. Safari moja Khalifa Mtukufu wa tatu alitoa matamshi Fulani juu ya baadhi ya wabashiri miongoni mwao alikuwemo yeye marehemu kuwa, hivi sasa wanaonekana wakitembea tembea katika mitaa ya m ji wa Rabwah, hakuna anayewauliza chochote na kutaka kuelewa chochote, lakini hawa ndio wale watu ambao ni wabashiri wan chi hizo na wakiwa huko maraisi wan chi na mawaziri hukutana nao hawa hualikwa katika dhifa na hadhara mbalimbali, huheshimika sana na hupewa hadhi kubwa. Marehemu aliporudi kutoka nchini Kenya akamwandikia barua rafiki yake mmoja kuwa mimi nimekaa miaka karibu ishirini na tisa Afrika, daima mimi nimejikuta sina uwezo wa kuitumikia dini vizuri kama inavyostahili, mara nyingi nilikuwa naamka usiku saa nane na baada ya kutafakari juu ya hali yangu ya udhaifu ya kutoweza kutekeleza majukumu yangu vyema nilikuwa nafadhaika sana, nilikuwa nasali tahajjud na namuomba sana msaada Mwenyezi Mungu na kisha nilikuwa naandaa ratiba ya kesho. Hivyo basi, wabashiri wetu wote wanatakiwa waziweke fikra zao juu ya njia hizi. Wawe na jazba za utumishi kama hii, wawe na uchungu daima wafanye maombi kwa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Awajaalie wabashiri wote watimize waqfu wao kwa uaminifu, waweze kutekeleza utumishi wao vizuri na Mwenyezi Mungu Ainue pia daraja za marehemu Sheikh Sharma. Vivyo hivyo, baada ya mgawanyiko wa India na Pakistan wakati wa uhuru kama ilivyokuwa maeneo mengine nchini India, mjini Qadian pia kulitokea vurugu nyingi wakati huo, baba yake

na kaka zake marehemu walikuwa huko, marehemu Sheikh Sharma akamwandikia barua baba yake na kaka yake pia kuwa ninyi watu mnabahati nzuri kuwa mko huko. Mimi pia napenda hivyo, hali ilivyo ni kwamba maisha hayana uhakika na hayatabiriki kuwa nani atarudi salama au hapana. Lakini kufa pia kwa ajili ya dini kuna heshima yake, laiti mimi ningekuwa huko basi kifo hiki cha ushahidi ningekipata, lakini ninyi wenzangu mlioko huko msije mkaogopa, maana uhai huja na kutoweka, Allah Awajaalieni kuyalinda makao makuu.

Hizi ndizo zilikuwa jaziba zake alizoziandika, wakati huo amerudi huyu marehemu alikuwa mtu mwema sana mukhlis. Pale alipokuwa na uwezo wa kutembea alikuwa na kawaida ya kunitembelea. Alipokuwa hawezi basi alitumia kiti cha kusukuma na tulikuwa tukionana. Alikuwa akija kusali sala ya Ijumaa katika msikiti wa Alfazal. Nilipokuwa napanda gari la kunileta huku Baitul Futuuh yeye mara zote alikuwa anakaa kwenye kiti chake cha kusukuma huku uso wake ukidhihirisha mng'ao wa upendo na uchangamfu. Tulikuwa tukionana na kusalimiana. Hata baada ya hapo pia mjukuu wake alieleza kuwa alikuwa na mahusiano makubwa sana na nidhamu ya Ukhalifa. Mjukuu wake huyu amejitolea maisha yake pia na hivi sasa yeye ni mubashiri huko Sweden Mwenyezi Mungu Mtukufu Amjaalie yeye pia aweze kufuata nyayo za marehemu babu yake". Amin.

Baada ya maelezo ya Hadhrat Amirul Mu'miniin Khalifatul Masihi – V (a.t.b.a) ni dhahiri kuwa Maulana Sheikh Sharma akawa ameingia katika utumishi wa Jamaat na ndipo akaanza safari ya kumtumikia Mwenyezi Mungu. Alisafiri kwa meli kutoka Mumbai India na akawasili Dar es salaam tarehe 05th March, 1949.
ARUSHA. Baada ya kuwasili Dar es salaam yeye akapangiwa kufanya kazi Arusha ambapo alibahatika pia kusimamia Moshi na vitongoji vyake. Huko Moshi aliwahi kuwatembelea viongozi wa dini na serikali akiwemo chifu Mangi Mkuu wa Wachaga Thomas Mareale ambao aliwafikishia ujumbe wa dini ya Islam na kuwatambulisha kwa kirefu juu ya Silsila ya Ahmadiyya Muslim Jamaat. Ingawa wengi hawakuafikiana nae juu ya tofauti za misingi ya dini, lakini walikubali kuwa dini ya Kiislam ni dini yenye mafundisho mazuri na yanampeleka mtu karibu na muumba wake.

Siku zile hali ya maendeleo ilikuwa duni nae mara zote

alikuwa anasafiri kwa magari ya kawaida na hakuona ajizi kutumia hata malori kwa usafiri wa kawaida. Siku moja alikuwa anasubiri usafiri ambao hakutegemea kuupata kwa vile ilionekana amechelewa kupata usafiri uliozoeleka kwa wageni gari ya abiria. Lakini bila kukata tama aliendelea kubahatisha usafiri huku akiongea na watu, basi ghafla akaona gari moja limesimama na alipolisogelea akaona kumbe ni gari la Mkuu wa Jimbo (Provincional Commissioner) akasita kulielekea, lakini mara akaitwa na Mkuu huyo na baada ya kueleza kuwa alikuwa akisubiri usafiri wa kuelekea Arusha, Mkuu huyo akamkaribisha akae ndani ya gari na hivyo akawa amepata msaada maalum wa Mwenyezi Mungu.

MIJADALA YA DINI

Alipokuwa Arusha alifanya mijadala ya dini ya watu mbali mbali, wakiwemo Waislam na Wakristo pia. Safari moja alipata nafasi ya kufanya majadiliano ya kidini na Mkuu wa shule ya Sekondari ya Kilutheri. Yule Mwalimu Mkuu akafurahishwa sana na uchangamfu wa marehemu Sheikh Sharma na akasema kuwa anatoa hoja za msingi kabisa juu ya dini ya Kiislam. Safari moja pia akikutana na mchungaji wa Kirusi Dr. Ruushi, wakajadiliana naye juu ya ubora wa mafundisho ya dini mbili kubwa, za Kiislam nay a Kikristo. Vile vile aliwahi kukutana mara kadhaa na Mujtahid (Sheikh) wa Kishia na kuongea nae maswala ya tofauti baina ya Ukhalifa wa Hadhrat Ali (ra) na Makhalifa waliomtangulia yaani Hadhrat Abubakar, Hadhrat Omar na Hadhrat Uthman (ra). Akiwa huko Jamaat ya Waumini wa Kiahmadiyya yalipatikana.
Akiwa hapa Tanganyika katika kazi za Mahubiri alikutana na watu maarufu akiwemo chifu Adam Sapi Mkwawa na Chifu Kidaha Makwaiya. Hawa wote alipokutana nao aliwaelezea juu ya habari za Jamaat Ahmadiyya na jinsi inavyofanya kazi ya Mahubiri duniani kote. Alipokuwa Mombasa kwa fadhili ya Allah vijana watatu wa Kiarabu walijiunga na Jamaat. Kipindi hicho hicho Jamaat za Taveta zilianzishwa. Safari moja huko Taveta akaalikwa na chama cha Theosophical kutoa hotuba juu ya Uislam na ukweli wa Wahyi, lilileta athari nzuri na baada ya maswali watu walielewa juu mafundisho ya Islam. Akiwa huko Mombasa alitembelea Lamu na Walimu na Masheikh mbalimbali wa kisunni aliwastaajabisha sana kwa ujuzi wa elimu ya dini aliyokuwa nayo Sheikh Sharma Sahib.

Aliwahi kwenda Zanzibar wakati wa vuguvugu la kupigania uhuru. Huko alikutana na viongozi mbalimbali na kuwafikishia ujumbe wa Ahmadiyya. Akiwa Mombasa aliwahi kukutana na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na wakaongea kwa kirefu juu ya haki za kupata uhuru wa kujiamulia mambo yao wenyewe. Aliwahi pia kutembelea Songea, Tunduru, Masasi, Mtama na Lindi. Katika harakati hizo aliwahi pia kutembelea Morogoro, Iringa na sehemu Fulani huko Mbeya ambapo baada ya kuwahubiria watu waliathirika na wengi wakajiunga na Jamaat ya Waislam wa Ahmadiyya. Hata hivyo kutokana na juhudi zake Jamaat kubwa ilipatikana hasa kule Asembobay, watu makini sana walijiunga na Uislam, hasa kwa vile Wakristo wa madhehebu mengi sana ndiyo Makao yao, marehemu Shehikh Sharma akiwa jimboni Tanga alifanya mahubiri sehemu zote maarufu hasa kule kwenye milima ya Usambara hasa Korogwe, Handeni, Pnagani na Mombo na Lushoto. Huko Mapadri walijenga hila na wakamshitaki kwa D.C azuiwe kuhubiri lakini walishindwa vibaya katika mpango nae aliendelea na kazi yake ya kueneza neno la Mungu.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Safar/Rabiul 1 1435 AH | January 2013 | Sulh 1393 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Abdullah bin Amr (ra) anasimulia kwamba mtu mmoja alimuuliza Mtume s.a.w kitu gani ni bora zaidi katika Islam? Akajibu uwalishe chakula watu wenye haja na uwatolee salamu ambao unawafahamu na usio wafahamu (mradi kila mtu). -(*Bukhari na Muslim*)

Wasifu wa Maulana Sheikh Abdulkarim Sharma

Na Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya – Songea

Tumepokea kwa huzuni kubwa taarifa kuwa mmoja wa Masheikh hodari walioitumikia Ahmadiyya Muslim Jamaat Afrika Mashariki Maulana Sheikh Abdul Karim Sharma amefariki dunia hivi karibuni huko London Uingereza. Innaalillahi wa Innailaihi Rajiuun – Sisi ni wa Allah na bila shaka kwake tutarejea.

Kabla ya kuendelea na maelezo ya maisha yake na utumishi wake ndani ya Jamaat ya Waislam wa Ahmadiyya napenda niandike maelezo aliyoyatoa Hadhrat Amirul Muminiin Hadhrat Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa tano Mungu Amsaidie kwa msaada wenye nguvu kabla ya kutangaza swala ya jeneza ya marehemu Sheikh Abdulkarim Sharma, maelezo hayo Huzur aliyatoa mwishoni mwa hotuba ya Ijumaa aliyotoa tarehe 12 Julai 2013 katika Msikiti wa Baitul Futuuh mjini London.



Kutoka kushoto Bw. Saidi Manoro, Sheikh AbdulKarim Sharma, Sheikh. Abdul Wahab walipokutana nchini Uingereza wakati wa Jalsa Salana ya mwaka 2008

Huzuralisemakuwakunajeneza jingine la ghaibu pia nalo ni la Maulana Sheikh Abdulkarim Sharma aliyefariki wiki chache zilizopita na tayari mazishi yake yamekwishafanyika, marehemu alizaliwa tarehe 26 Mei 1918 mjini Qadian India. Baba yake aliitwa Mzee Abdul Rahim alitokana na wahindu na Abdul Rahim sahaba wa Sayyidna Ahmad (as) aliachana na dini ya Kihindu na akajiunga na Uuislam kwa mkono wa Hadhrat Masihi Mauud mwaka 1904. Mama mzazi wa marehemu Sheikh Sharma alikuwa Bi. Aisha Begum sahiba. Mama huyu alilelewa na Hadhrat Ummul Muuminiin mkewe Sayyidna Ahmad (as) na aliwahi kuwanyonyesha watoto wa Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad Khalifatul Masih wa pili (ra) na watoto wa Hadhrat Mirza Sharif Ahmad (ra) pia. Hivyo akawa pia ni mama yao wa kunyonya. Bibi yake mzaa baba yake marehemu ambaye nae pia alikuwa mhindu alijiunga na Uislam. Babu mzaa mama wa Sheikh Abdulkarim Sharma Hadhrat Karam Dad Khan alikuwa sahaba wa Hadhrat Ahmad (as). Vivyo hivyo bibi yake mzaa mama yake Sahiba pia alikuwa mama wa kunyonya wa Hadhrat Mirza basher Ahmad, watoto wawili wa kaka yake marehemu Be. Abdul Rashid Sharma mabwana Sheikh Muzaffar Ahmed na Sheikh Mubarak walipata pia heshima ya kuwa mashahidi kwa kuuawa kwa ajili ya dini.

Endelea uk. 11

Mwalimu Nyerere na Waahmadiyya

Na Mahmood Hamsin Mubiru - Dar es salaam

Mwenye nia ya kweli na dhati yenye ithibati ya kuandika m aisha ya MwalimuJulius Kambarage Nyerere hana budi kuongeza ukurasa ambao atauita 'Nyerere na Waahmadiyya'. Tunaelewa ukurasa huo utakuwa mgumu na utafiti wa kina utahitajika na hapa tunajitahidi kumsaidia Mwandishi huyo.

Maisha ya kisiasa ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere yameathiriwa kwa kiwango fulani katika kukutana na kushirikiana na Wanajumuiyya. Tutatoa mifano na kuthibitisha hoja hiyo kutokana na kufahamiana kwa Mwalimu Nyerere na wafuasi wafuatao wa Jumuiyya ya Ahmadiyya ambao ni Maulana Sheikh Mubaraka Ahmad (HA), Hassan Toufiq, Sheikh Abdulkarim Sharma, Sheikh Inayatullah Ahmad, Sheikh Jamil Rahman Rafiq, Sheikh Muhammad Munawwar, Sir Muhammad Zafrullah Khan, Jumanne Abdallah, Sheikh Kaluta Amri Abedi na Dr. Abdussalaam.

Tunaanza na Sheikh Mubarak Ahmad (HA) ambaye alikuwa Mbashiri wa kwanza wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya Afrika Mashariki aliyezaliwa tarehe 10/10/1910 alipata shahada yake katika lugha ya Kiarabu na akatoa maisha yake yote kutetea na kuhubiri dini tukufu ya Islam. Mwaka 1934 alitumwa na Khalifatul Masih wa pili Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad kuja Afrika Mashariki. Kituo chake cha kwanza kilikuwa Mombasa na baadae akapata mwaliko na Waahmadiyya wachache waliokuwa Tabora aende huko. Kama ilivyo desturi ya Mwanachuoni huyo wa Kiislam alifanya utafiti, utafiti huo ukabainisha mambo matatu. Kwanza Tabora ulikuwa ni uwanja wa madhehebu mengi ya Kikristo. Pili Tabora kilikuwa ni kituo kikubwa cha Islam na jmbo la tatu palikuwa pamejengwa chuo kikuu cha kutengeneza Mapadri kinachoitwa Kiparapara. Shekh Mubaraka Ahmad alionelea mapambano yaanze pale pale penye kitovu cha kuwatayarisha Mapadri. Na mwisho palikuwa na shule maarufu ya Wavulana Tabora (Tabora boys). Shule ambayo historia inaonyesha baadae ilikuja kuwatoa viongozi wengi wa Tanganyika huru. Kutokana na sababu hizi Sheikh Mubaraka Ahmad alifika mjini Tabora na Novemba 1934 akasajili rasmi Jumuiyya ya Ahmadiyya.

Zipo kazi nyingi alizozifanya katika siku zake za mwanzoni kama kuanzisha gazeti la Mapenzi ya Mungu, Kuanza kazi ya kutafsiri Qur'an Tukufu kwa Kiswahili, kutafuta kiwanja kwa ajili ya kujenga Msikiti, kwa ajili ya mada yetu hii tutaweka mkazo juu ya shule ya wavulana ya Tabora (Tabora boys). Kutokana na uchangamfu wake na bashasha na mapenzi ya kuwapenda watu Sheikh Mubaraka Ahmad kwa muda mchache aliwapata marafiki wengi na mmoja wa marafiki zake alikuwa ni Mwalimu Mkuu wa Shule ya wavulana ya Tabora aliyeitwa Blummer. Mwalimu Mkuu huyu alivutiwa na elimu aliyokuwa nayo Sheikh Mubaraka pamoja na ufasaha wake wa lugha ya Kiingereza na hivyo akamkaribisha pale shuleni Tabora ili aweze kuwafundisha watoto wa Kiislam ambao hawakuwa na Mwalimu wa dini.

Kuwasili kwa Sheikh Mubaraka Ahmadi katika shule hiyo ya Tabora ya wavulana kulileta msisimko wa aina yake. Sheikh Mubaraka Ahmad alipewa fursa ya kufundisha dini ya Islam. Somo lake la kwanza kuhusu Islam kuliwasisimua wengi na aliyoyasema yakawa gumzo bwenini. Alieleza umoja wa Mwenyezi Mungu



(Katikati mbele) Mwalimu Nyerere katika msikiti wa Ahmadiyya (Masjid Salaam, Dar es Salaam mwaka 1958)

unavyoelezwa na Islam, usawa unaopatikana Msikitini ambapo watu hawakai kufuatana na vyeo vyao isipokuwa mtu aliyewahi na usawa mkubwa wa binadamu na heshima ya binadamu pia ambavyo hivyo vyote havitokani na rangi wala kabila isipokuwa Ucha Mungu. Alieleza pia kuwa ya kwamba binadamu ameumbwa yuko huru na si sawa sawa mtu yeyote mwingine kumuweka katika hali ya utumwa, kumuonea, au kumnyanyasa. Mmoja wa wanafunzi waliopata msisimko wa ajabu ni Julius Kambarage Nyerere. Maelezo hayo aliyotoa Sheikh Mubarak Ahmad ndio kwanza walikuwa wameyasikia. Alipokuja safari ya pili Nyerere alikuwa miongoni mwa wanafunzi wa mwanzoni kufika darasani. Ikumbukwe ya kwamba Sheikh Mubaraka Ahmad alipoanza kufundisha pale Tabora aliwaruhusu watu

Endelea uk. 10